SportPesa
TZS. 861,636,800
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wanafunzi** Lucky Vincent waliopata ajali wafanya maajabu kidato cha IV

UKURASA 3



**JUVE YAKATAA KUMSAJILI MARTIAL**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Januari 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580831

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




KESI YA MBOWE

# Marufuku majina ya JPM, Samia kutajwa

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MHUDUMU 'GESTI' AUAWA KINYAMA**

MHUDUMU wa nyumba ya kulala wageni ya Peace Lodge iliyoko Matarawe...

UKURASA WA 4

**SABAYA ADAI MASHTAKA DHIDI YAKE YAMELENGA KUMCHAFUA**

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amedai mashtaka...

# Marekani yaipatia Tanzania dozi mil.1.6 chanjo ya UVIKO

UKURASA 5



Mwananchi akipita kwenye nguzo zilizowekwa mbadala baada ya daraja linalounganisha eneo la Mwembe Kiboko Kata ya Kinyerezi na Kifuru Tabata, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii kuharibiwa na mvua na kusababisha hatari na usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo, hasa wazee na watoto. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Dalili moshi mweupe Uspika CCM kuanza kuonekana rasmi

UK.2

**MICHEZO** YANGA : LIGI KUU 'NGOMA MBICHI' UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Mhudumu 'gesti' auawa kinyama

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MHUDUMU wa nyumba ya kulala wageni ya Peace Lodge iliyoko katika eneo la Matarawe Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ambaye jina lake limehifadhiwa anayekadiliwa kuwa na umri wa miaka 23 amekutwa amekufa kwenye moja ya vyumba vya kulala wageni.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Louis Taisamo, alisema tukio hilo limetokea juzi jioni ambako inadaiwa kuwa kwenye nyumba hiyo chumba namba nnne mhudumu huyo, mkazi wa Kimoro-Makambi Manispaa ya Songea alikutwa akiwa ameuawa kwa kukabwa shingoni na kamba ya viatu na mtu asiyefahamika kwa jina, ambaye alikuwa ni mpangaji katika chumba hicho.

Alisema inadaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alipanga chumba namba nne kwa siku tano kuanzia Januari 6, mwaka huu hadi Januari 10 mwaka huu na baada ya hapo alitoweka na hakuwa analala katika chumba hicho.

Kamanda Taisamo alifafanua kuwa inadaiwa mtuhumiwa huyo alitoweka kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni baada ya kuwa na deni la pango Sh. 50,000 ambapo alilazimika kuacha simu yake aina ya Nokia na baadhi ya nguo zake mpaka hapo atakapolipa deni.

Alieleza zaidi kuwa inadaiwa mtuhumiwa huyo alikuwa akifika katika nyumba hiyo ya wageni mara kwa mara kuomba arudishiwe simu na nguo zake na alikuwa akijibiwa na mhudumu (marehemu) kuwa mali zake zipo kwa mmiliki wa nyumba hiyo na kwamba atarudishiwa mali zake baada ya kulipa deni.

Alisema inadaiwa siku ya tukio mtuhumiwa ambaye jina lake halijafahamika, alifika tena kwenye nyumba hiyo na kuwasiliana na mhudumu ambapo baada ya kutekeleza mauaji alitoroka na kufanikiwa kuondoka na vitu vyake ambavyo vilikuwa vimezuiliwa.

Taisamo alisema mtuhumiwa hajakamatwa, na kwamba Jeshi la Polisi mkoani humo linafanya juhudi za kumtafuta.

### KESI YA MBOWE

# Marufuku majina ya JPM, Samia kutajwa

**Na Kulwa Mzee**

JAJI Joackim Tiganga anayesikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu amesitisha maswali ya wakili wa utetezi yanayomtaja Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli na Rais Samia Suluhu katika kesi hiyo wakati hawapo kortini.

Maswali hayo ya kutaja Rais wa awamu ya tano na sita yaliibuliwa jana na wakili wa utetezi, Faraja Mangula, wakati akimuhoji shahidi wa 10 wa Jamhuri, Inspekta Innocent Ndowo, kutokana na ushahidi wake.

Wakili Mangula alihoji swali akitaka shahidi aeleze cheo cha Inspekta alikipata wakati wa Rais wa awamu ya tano au ya sita.

Akijibu shahidi alidai haelewi swali lake ndipo Jaji Tiganga alipomuhoji wakili huyo kuwa swali la nani alikuwa Rais anataka kujenga kitu gani.

Wakili Mangula alidai anataka kujenga msingi, lakini Jaji alihoji huo msingi ndio atengeneze kupitia Rais aliyekuwapo madarakani.

"Nilishatoa maelekezo ya kutaja majina ya watu ambao hawapo mahakamani, lakini nataka kujiuliza kuhusu kuuliza maswali ya Rais wa awamu ya tano au la unachotaka hapo ni nini? Alihoji Jaji Tiganga.

Wakili Mangula alidai katika kesi hiyo kuna watuhumiwa walikamatwa awamu ya tano na wengine awamu ya sita, lakini aliomba kuuliza maswali kwa namna nyingine.

Shahidi alidai alipewa vielelezo zikiwamo simu kufanya uchunguzi na hajui kama kuna ugaidi au hakuna.

Inspekta Ndowo alidai katika simu kulikuwa na mazungumzo ya watuhumiwa na mazungumzo ya muda mrefu yalikuwa dakika tisa na alipohojiwa sauti zao ziko wapi aliomba asijibu swali hilo kwa sababu za kiusalama.

Shahidi anadai wakati wanafanya uchunguzi hawakuwa na maslahi na kesi hiyo, hivyo si sahihi kwamba waliamua kuficha baadhi ya taarifa katika kesi hiyo.

Akihojiwa na Wakili Fredrick Kihwelo kuhusu kampuni ya Celebrite anayodai inatengeneza software kwamba ni kampuni ya kijasusi ya kidigitali ya nchi ya Israeli alidai hafahamu.

Alidai hafahamu kama kampuni hiyo pia inahusishwa na unyanyasaji wa waandishi wa habari na wanaharakati duniani.

Akihojiwa na Wakili John Mallya alidai kielelezo C ni simu ya mshtakiwa Halfani Bwire ambayo katika uchunguzi hakukuta kitu cha kuchukua.

Anadai ujumbe wenye matokeo hasi alioukuta hakuwa na sababu ya kuuweka.

Anadai alifanya uchunguzi Julai 2021, ushahidi amekuja kutoa Januari 2022 ni takribani miezi mitano.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020.



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, wakiwa wametundika bidhaa zao kwenye uzio wa kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya serikali kuwaondoa katika maeneo hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dalili moshi mweupe U-spika CCM kuanza kuonekana rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

JOTO la uchaguzi wa spika ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) linazidi kupanda kutokana na kitendawili cha wanachama watatu kati ya 71 waliojitokeza kuomba nafasi hiyo kufanyika leo.

Awali kikao cha Kamati Kuu ya CCM, kilipangwa kufanyika juzi, lakini kikasogezwa hadi leo. Kamati Kuu inatarajiwa kutoa majina matatu ya wanachama watakaopigiwa kura na wabunge wa chama hicho, kumrithi Job Ndugai, aliyejiuzulu hivi karibuni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, kikao hicho kitafanyika Makao Makuu ya CCM, Dodoma.

"Kikao hicho kitatanguliwa na kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Maandalizi ya vikao vyote hivyo yamekamilika," alisema Shaka.

Kwa mujibu wa ratiba ya awali, uchukuaji fomu ulimalizika Januari 15, ukafuatiwa na kikao cha Sekretarieti Januari 17 na sasa ilisubiriwa kikao cha Kamati Kuu.

Baadhi ya makada waliojitokeza ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mbunge wa Bariadi Magharibi, Andrew Chenge, aliyekuwa Katibu wa Bunge, Dk. Thomas Kashililah, aliyekuwa Waziri na Mwenyekiti wa UWT, Sophia Simba.

Wengine ni aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Bunge la Afrika (PAP) na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele na msomi aliyejinasibu ana shahada tisa, Baraka Byabato na Mbunge wa Geita, Joseph Kasheku maarufu kama Msukuma.

HABARI KITAIFA

# M'biashara kortini madai kutakatisha Dola 150,000



Mfanyabiashara Oliver Nantocha maarufu Mohammed Nantocha au Joshua Kaisi (kushoto), akiwa chini ya ulinzi wa askari kanzu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka sita ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha Dola za Marekani 150,000 alizozipata kwa njia ya udanganyifu wa kusambaza dhahabu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Kulwa Mzee**

MFANYABIASHARA Oliver Nantocha, maarufu Mohammed Nantocha au Joshua Kaisi, amepanda kizimbani akikabiliwa na mashtaka sita ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha Dola za Marekani 150,000 alizozipata kwa njia ya udanganyifu kwa kusambaza dhahabu.

Mshtakiwa alipanda kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga. Akisomewa mashtaka na Wakili wa Serikali Mkuu, Veronica Matikila, inadaiwa Januari 17, 2020 kwa udanganyifu mshtakiwa alighushi nyaraka/risiti ya kuhifadhi kwa lengo la kudanganya kuwa Kampuni ya Lockfort Security Company Limited imepokea kilo 100 za dhahabu kutoka kwa Samuel Kabula, wakati akijua sio kweli.

Katika shtaka la pili inadaiwa kabla ya Machi 5, mwaka 2020 Dar es Salaam, mshtakiwa alighushi mkataba wa mauziano kati ya Cozac Logistics International Company Limited ya Tanzania na Innovative Perspective Company Limited ya Botswana kwa lengo la kuonyesha kuwa Kampuni ya Cozac Logistics International Company Limited imeingia mkataba wa kuuza dhahabu kilo 500 kwa kampuni ya Innovative Perspective Company (PTY) Limited kwa gharama ya Dola 27,000 kwa kila kilo wakati sio kweli. Katika shtaka la tatu inadaiwa kipindi hicho mshtakiwa alighushi nyaraka ya kuonyesha kuwa Kampuni ya Cozac Logistics International Company Limited, imeweka hati fungani ya kuuza kilo 450 ya dhahabu kwa Innovative Perspective Company (PTY) Limited wakati akijua sio kweli. Wakili Matikila alidai, shtaka la nne kuwa Septemba 18 mwaka 2020, mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa alighushi taarifa ya kuonyesha kuwa Kampuni ya Southern Eastern African Mineral Central (SEAMIC), imethibitisha kuwa kilo 60 zimethibitishwa kuwa ni dhahabu kwa asilimia 97.24 hadi 97.71 wakati akijua sio kweli.

Inadaiwa katika shtaka la tano kuwa kati ya Januari mosi, 2020 hadi Februari 12, 2021 alijipatia Dola za Marekani 150,000 kutoka kwa Emanuel Oteng Motilhatlhedi, mwakilishi wa Kampuni ya Innovative Perspective Company Limited baada ya kudanganya kuwa angewauzia kilo 500 za dhahabu wakati akijua sio kweli.

Katika shtaka la sita la utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Januari mosi, 2020 na Februari 12, 2021 mshtakiwa alitakatisha Dola 150,000 wakati akijua zilitokana na kosa tangulizi la kugushi.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa ambapo ilipangwa kutajwa Januari 31, mwaka huu.

Mshtakiwa alirudishwa rumande kwa kuwa kosa la utakatishaji fedha halina dhamana kisheria.

# Wanafunzi Lucky Vincent waliopata ajali wafanya maajabu kidato cha IV

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI watatu walionusurika kwenye ajali ya Shule ya Lucky Vincent, wamefanya maajabu katika mtihani wa kidato cha nne na kufaulu vizuri kwenye masomo ya sayansi.

Wanafunzi hao ni Doreen Elibariki ambaye amepata daraja la pili, Wilson Godfrey (daraja la kwanza) na Sadia Awadh (daraja la pili).

Akizungumza kwa furaha kwa njia ya simu ya kiganjani, mzazi wa Sadia, Zaituni Abdul, alisema katika matokeo hayo anamshukuru Mungu kuwapigania watoto wao.

"Hakika namshukuru sana Mungu maana kwa matatizo waliyopitia hawa watoto sikutegemea kama watapata matokeo haya, hakika furaha yangu kubwa sana," alisema.

Alisema mwanawe ndoto yake kubwa ni kuwa daktari wa binadamu au rubani.

Mama mzazi wa Doreen, Neema Mshana, alisema alipopata matokeo hayo alimuona Mungu akimshika mkono mwanawe na wenzake.

"Hakika Mungu mwema anajua waja wake na hajawaacha, naamini ataendelea kutembea na watoto hawa mpaka watakapofikia ndoto zao," alisema.

Mwalimu wa darasa wa wanafunzi hao, Pascal Safari, aliwapongeza watoto hao kupata ufaulu mzuri licha ya matatizo waliyopitia.

Alisema katika darasa lao walikuwa jumla ya wanafunzi 65 ambao kati yao 26 wamepata daraja la kwanza akiwamo Wilson, 30 walipata daraja la pili akiwamo Doreen na mwenzake Sadia.

Pascal alisema wanafunzi wengine nane walipata daraja la tatu na mmoja daraja la nne.

Alisema watoto hao ambao manusura ya ajali wote walikuwa mkondo wa sayansi na wamefaulu vizuri.

"Naamini watoto hawa wanaweza kurudi hapa shuleni kuendelea na masomo yao ya kidato cha tano na sita kwani mazingira yaliyoko mazuri yanawafaa kuendelea na masomo," alisema.

Wanafunzi hao walipata ajali ya gari Mei 6, mwaka 2017, wakati wakielekea kwenye Shule ya Tumaini Junior iliyoko wilayani Karatu kwa ajili ya kufanya mtihani wa kujipima.

Katika ajali hiyo wanafunzi 32, walimu wawili na dereva walifariki papo hapo eneo la Rhotia wilayani Karatu, huku wanafunzi hao watatu wakinusurika.

Baada ya ajali hiyo Shirika lisilo la kiserikali la STEMM chini ya mratibu wa safari hiyo, Lazaro Nyalandu, liliwasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo nchini Marekani, Steve Meyer, ambaye kwa ushirikiano na serikali waliwezesha kupatikana kwa hati ya kusafiria haraka kwenda nchini Marekani kwa matibabu zaidi baada ya kugundulika kuvunjika mara 36 mwilini mwao kila mmoja.

Doreen alilazimika kupelekwa kituo maarufu duniani cha Madona nchini Marekani, kutokana na tatizo la uti wa mgongo.

Agosti 18, mwaka 2017 walirejea nchini kwa msaada wa Shirika la Ndege la Mfuko wa Msamaria la Marekani linaloendeshwa na Frankline Graham, mtoto wa mwimbaji maarufu duniani, Bill Graham, wakiwa wameambatana na wazazi wao watatu na daktari bingwa wa mifupa wa Hospitali ya Mount Meru, Elias Mashalla na Dk. Siniphorosa Silalye.


CHAMPION Auction Mart

## MARUDIO YA NOTISI TANGAZO

**CHAMPION AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya taasisi ya kifedha ya **MWANGA HAKIKA BANK,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa Mdaiwa afuatae ndani ya siku saba kuanzia tangazo hili. Vinginevyo,tutafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha:

| NO. | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | JOSEPH MAGARYA BURANGA | NYUMBA-INA LESENI YA MAKAZI | KIPUNGUNI B | 27/01/2022 SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Mali itauzwa katika hali iliyopo.
4. **Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0682981090/ 0699364444**



Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora (katikati), akikata utepe wakati akikabidhiwa msaada wa jengo la madarasa mawili, matundu mawili ya vyoo na madawati 50 yaliyofadhiliwa na Tanzania Commercial Bank (TCB), katika Shule ya Msingi Kitunga, wilayani Muleba, mkoani Kagera. Wengine ni Mkurugenzi wa Biashara na Wateja Wakubwa wa TCB, Adolfina William (wapili kushoto), Mkurugenzi wa Mipango na Mikakati wa Benki hiyo, Muondakweli Kaniki (wapili kulia) na Mkuu wa Shule hiyo, Hashim Kibaiza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sabaya adai mashtaka dhidi yake yamelenga kumchafua

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amedai mashtaka ya uhujumu uchumi yaliyofunguliwa na Jamhuri dhidi yake yametengenezwa ili kumvunjia heshima na imani kwa Rais wa Tanzania.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili na mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31). "Makosa matano yaliyofunguliwa na mashtaka si ya kweli ni ya uongo yametengenezwa kwa misingi ya kisiasa ili kunivunjia heshima na imani kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania," alidai.

Sabaya alidai kuwa aliweka rehani maisha yake kwa kazi ya serikali mpaka akatumiwa watu wa kutaka kumuua.

Pia alidai kuwa Ofisa Uchunguzi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ramadhani Juma, alishindwa kufanya upelelezi wa kina dhidi ya mashtaka yanayomkabili na alipaswa kuwa upande wa serikali na si kutafuta genge la wafanyabiashara waseme walimpatia fedha.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, Sabaya alidai kuwa mashtaka hayo yametengezwa na wapambe wa mtu anayedhani kwamba alikuwa sehemu ya kumzuia kushinda kiti cha ubunge katika Jimbo la Hai, hivyo TAKUKURU hawakupaswa kujiingiza katika mchezo huo.

Pia alikuna kuunda kikosi kazi maalumu kilichodaiwa ni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na maofisa kutoka Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) kilichokwenda kwa mfanyabiashara Francis Mroso kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 90. Kadhalika, Sabaya alidai ushahidi uliotolewa na shahidi 11 wa mashtaka, Hemed Shaban, kwamba hakuwa na uhusiano mzuri na aliyekuwa Mkuu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ni uongo.

"Kilichozungumzwa hapa mahakamani na shahidi wa 11 wa Jamhuri ni uongo kwa kuwa aliacha kazi yake ya kufanya upelelezi na kujiingiza katika siasa za mkoa wa Kilimanjaro," alidai Sabaya.

Sambamba na hayo, alidai kwamba Ramadhani Juma, shahidi wa 13 wa mashtaka ameshindwa kufanya ushahidi na kujiingiza katika siasa na kwa wafanyabiashara wa Kilimanjaro kwa kuwa mtu wao alishindwa kwenye uchaguzi.

"Mheshimiwa Hakimu Mroso siyo shahidi wa kweli kwa kuwa alipokwenda kuripoti polisi Februari 11, alikuwa na umri wa miaka 47 na mwaka huo huo alipokuja hapa mahakamani alidai kwamba ana miaka 44," alidai. Shahidi huyo alikana madai ya kutakatisha Sh. milioni 90 na akitoa mgawo kwa vijana wake wakiwa katika Hoteli ya Tulia Lodge.

Alidai kwamba suala Mkuu wa Wilaya kununua gari ya Sh. milioni 60 ni jambo la kawaida kwa kuwa akifanya kazi miezi 14 tu anakuwa na kiasi hicho cha fedha ilhali yeye ametumikia nafasi hiyo kwa miezi 33.

"Kule Mkinga, Tanga, nina ng'ombe 1,400 niliopewa na wazazi wangu. Ukiuza ngombe 70 tu unapata fedha hizo. Nina shamba King'ori ekari 54 na Loksale nakodisha mashamaba niliyopewa na wazazi wangu," alidai.

# Mitambo ya visima kuingizwa nchini

**Na Frank Monyo**

SERIKALI inatarajia kuagiza mitambo mikubwa 25 ya kisasa ya uchimbaji visima na seti tatu za mitambo ya kujenga mabwawa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, katika Ofisi za Kitengo cha Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa zamani ikijulikana kama Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA), mkurugenzi wa kitengo hicho kilicho chini ya RUWASA, Simon Ngonyani, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wengi mjini na vijijini.

Pia alisema lengo lingine ni kutoa huduma kwa wananchi mjini na vijijini na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini.

Alisema kwa sasa wananchi na taasisi mbalimbali za umma na binafsi, wanatakiwa kukiamini kitengo hicho cha serikali katika kazi za uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa na kuacha kutumia watu ambao hawana utaalamu.

"Hivi sasa uchimbaji visima umeingiliwa na watu ambao ni vishoka. Lazima tuwaambie wananchi pamoja na taasisi ambazo zinahitaji huduma ya kuchimbiwa visima kuwa hawana sababu ya kutangatanga mitaani waje kwenye kitengo chetu tuwapatie huduma. Kitengo chetu kina wataalamu wa kutosha wenye uwezo wa kazi hiyo," alisema Ngonyani.

Alisema mwaka jana walipewa kazi na Wizara ya Maji ya kuchimba visima 500 lakini walishindwa kukamilisha kazi hiyo kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwamo mitambo ila kwa mwaka huu wanaimani watafanikiwa kuchimba visima zaidi baada ya serikali kuagiza mitambo hiyo.

Ngonyani alitahadharisha wananchi, taasisi za umma na serikali kuacha kutumia vishoka kwa kuwa hawana utaalamu.

"Kwa mfano ukiangalia kwa hapa Dar es Salaam, utakuta visima vingi vimechimbwa karibu na miundombinu ya majitaka na kusababisha magonjwa ya milipuko. Kumbe watu wanatumia maji yanayoingiliana na mfumo wa maji machafu," alisema.

"Katika kukabiliana na uchimbaji wa holela wa visima, tutashirikiana na wenzetu wa mabonde ya maji kwani wao ndio wanaotoa vibali vya uchimbaji. Lakini ni vizuri wananchi wakafuata wataalamu wenye weledi kutoka kitengo chetu ili wapate huduma bora," alisema.

Aliongeza kuwa gharama za uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa ni nafuu, hivyo wananchi wasisite kufika katika ofisi hizo kwa ajili ya kupatiwa huduma kwa kuwa lengo la serikali ni wananchi kupata huduma ya maji safi kila sehemu.

# Askari sasa kusindikiza mabasi ya abiria

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, linaanza utaratibu wa kutumia askari wake kusindikiza mabasi ya abiria ili kukabiliana na ajali zinazotokana na mwendo kasi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Onesmo Lyanga, alibainisha hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ajali ya basi la abiria la kampuni ya Baraka Classic lenye namba za usajili T967 DWW, iliyotokea eneo la Pandambili, wilayani Kongwa, mkoani Dodoma.

Katika ajali hiyo watu watatu walifariki dunia na wengine 11 kujeruhiwa.

Kamanda Lyanga, alisema ili kukabilina na ajali zitokanazo na mwendokasi wa madereva wa mabasi ya abiria Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, linapanga kuanza kutumia askari kusindikiza mabasi ya abiria yaendayo mikoani.

"Kuanzia sasa katika mkoa wetu wa Dodoma tutaanza kutumia askari kusindikiza basi ambalo litakuwa la kwanza kuondoka stendi asubuhi na ni marufuku kwa mabasi yatakayotoka nyuma kulipita basi hilo hii itasaidia kudhibiti masuala ya mwendo kasi kwa madereva wa mabasi," alisema Kamanda Lyanga.

Akizungumzia tukio la ajali hiyo katika eneo la tukio Kamanda Lyanga, alisema basi hilo ambalo lilikuwa likitoka Dodoma kwenda Dar es Saalam, chanzo ni mwendo kasi licha ya kuwapo hali ya hewa ya mvua.

Alisema kuwa basi hilo lilipata ajali kutokana na mwendo kasi hali ambayo ilisababisha kupoteza mwelekeo na kwenda kukita katika kingo ya barabara.

"Hali ya barabara haikuwa mbaya sana, lakini chanzo ambacho kimesababisha ajali hii ni mwendo kasi wa dereva wa basi hili na watu 11 wamejeruhiwa na wengine watatu wamepoteza maisha," alisema.

Kadhalika, alisema kati ya watu hao watatu waliofariki, wawili wameshatambuliwa na miili yao imehifadhiwa katika Hopitali ya Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro.

"Kati ya hawa watatu waliofariki mmoja ametambulika kwa jina la Salha Mohamed, mwanafunzi wa kidato cha pili, mkazi wa Dar es Saalam na Joyce Nyaula, mtu mzima naye mkazi wa Dar es Saalam, huyo mmoja bado hajatambuliwa," alisema Kamanda Lyanga.

Vilevile, alisema majeruhi 10 wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya Kongwa kwa ajili ya matibabu na mmoja wao amekimbizwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa matibabu zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, aliwataka wananchi wanaotumia usafiri wa mabasi kutoa taarifa za madereva wanaoendesha vyombo vya moto kwa mwendo kasi.

"Kwa madereva sasa ni msimu wa mvua, hivyo wawe makini, lakini pia viongozi wa maeneo ambayo yapo jirani na barabara kuu kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa za ajali pindi zinapotokea," alisema Emmanuel.

# Mtanzania atwaa tuzo haki za binadamu

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI ya Ujerumani na Ufaransa jana imekabidhi tuzo ya haki za binadamu kwa Mtanzania, Noellah Msuya, kupitia taasisi yake ya kusaidia watoto wasiojiweza na wenye uhitaji maalumu ya 'Child Support Tazania' (CST).

Tuzo hiyo imetolewa baada ya serikali hizo kutambua mchango wa Noellah pamoja na taasisi yake hiyo kwa watoto zaidi ya 600 wanaowasaidia.

Akizungumza wakati wa kukabidhi tuzo hiyo kweye hafla iliyofayika nyumbani kwa balozi wa Ujerumai nchini Tanzania, Balozi Regine Hess, alisema kuwa tuzo hiyo imetolewa na serikali za nchi hizo kupitia kwa mawaziri wao wa mambo ya nje, Annalena Baerock na wa Ufarasa Jean-Yves Le Drian.

Alisema kila mwaka Desemba 10, Siku ya Haki ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, Ujerumani na Ufaransa, hutoa tuzo hiyo kuthamini mchango na juhudi za taasisi na mtu mmoja mmoja kwenye kusaidia wengine kupata haki zao.

"Tuzo hii imetolewa kwa taasisi na watu binafsi 15 tu duniani na kwa bahati nzuri Tanzaia ni miongoni mwa nchi iliyopata tuzo hiyo, tunampongeza Noellah na taasisi yake kwa tuzo hii," alisema balozi Regine Hess.

"Noelah na Taasisi yake wanatoa haki za msingi kwa watoto wenye ulemavu, haki hizo ni pamoja na kupata elimu na mahitaji mengine," alisema Regine.

Balozi Regine alizitaja nchi nyingine zilizotoa washindi wa tuzo hiyo kuwa ni Afghanistan, China, Haiti, Ufilipino, Iran, Lebanon, Uturuki, Afrika Kusini, Nigeria, Venezuela, Benin, Myanmar, Bosnia na Tanzania.

Aidha, kwa upade wake Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui, alimpongeza Noellah na kumtaka kuendeleza juhudi zake za kusaidia watoto wasiojiweza na wenye uhitaji.

Akizugumza wakati akipokea tuzo hiyo, Noellah ambaye ni Mkurugezi Mtendaji wa CST inayojishughulisha kuwasomesha na kuwasaidia watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali, alisema tuzo hiyo imempa moyo wa kuendelea kupambana kuwasaidia watoto wenye uhitaji.

"Wakati naanza sikutegemea kama mchango wangu utathaminika hivi, nawashukuru wadau wote ninaoshirikiana nao ikiwamo serikali ya Tanzania."





TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.

@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422


# Marekani yaipa Tanzania dozi mil. 1.6 chanjo corona

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI ya Marekani imetoa dozi milioni 1.6 za chanjo ya UVIKO-19 aina ya Pfizer BioNTech kwa Tanzania, kwa ajili ya kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Chanjo hizo zilikabidhiwa jana na Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya ya Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Ananthy Thambinayagam, na kupokewa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, aliyewakilisha serikali.

Hafla fupi ya makabidhiano ya chanjo hiyo yalifanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA). Dozi hizo ni sehemu ya dozi milioni 4.5 za chanjo dhidi ya ugonjwa huo ambazo serikali ya Marekani imeipatia Tanzania mpaka sasa.

Dozi hizo zimetolewa kupitia Mpango wa Kimataifa wa Usambazaji Chanjo wa COVAX, ikiwa ni jitihada za kulitokomeza janga hilo duniani. Mkurugenzi huyo alisema msaada huo ni kutimiza ahadi ya Rais wa Marekani, Joe Biden, kuwa Marekani itakuwa ghala la dunia la chanjo dhidi ya UVIKO-19 katika mapambano ya pamoja dhidi ya janga hilo.

"Tutaendelea kufanya kila linalowezekana kuifanya dunia kuwa mahali salama dhidi ya kitisho cha magonjwa ya kuambukiza," alimnukuu Rais Biden katika kauli yake aliyoitoa mwanzoni mwa mwaka huu. Shehena ya kwanza ya dozi milioni moja za Johnson and Johnson (J&J) ilipokewa Julai, mwaka jana, huku zaidi ya dozi milioni 3.5 za chanjo aina ya Pfizer BioNTech zikitolewa kwa awamu tatu kati ya Novemba, mwaka jana na Januari, mwaka huu.

"Msaada wa Marekani katika jitihada za kimataifa za kukabiliana na UVIKO-19 unajumuisha kuchangia dozi milioni 365 za chanjo kwa nchi nyingine. Kununua dozi bilioni moja za chanjo na kuzitoa kwa takriban nchi 100 zinazoendelea,"alisema Thambinayagam.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo wa USAID, Marekani pia itachangia Dola za Kimarekani bilioni 4 kusaidia COVAX.

Alisema lengo ni kusambaza chanjo dhidi ya UVIKO-19 duniani kwa usawa na ufanisi na kusambaza dawa muhimu na vifaa tiba, pamoja na kuzisaidia nchi kujenga upya uchumi wao, kukabiliana na upungufu wa chakula na kuimarisha usalama wa afya.

# Kibano zaidi kwa madereva

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi limeanza kutumia mashine mpya za kidijitali za kulipia tozo mbalimbali ambazo zinalenga kutatua changamoto na malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wananchi hususani wanaotumia vyombo vya moto.

Kupitia mashine hizo mpya, pia madereva wote watakaobainika na makosa barabarani kwa sasa wataanza kuchukuliwa alama za vidole.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na Msemaji wa Jeshi hilo, David Misime, kuanza kutumia mashine hizo kutaondoa malalamiko hayo ambayo yamekuwa yakitolewa.

"Kama mnavyokumbuka, serikali ilitoa maelekezo ya ukusanyaji wa maduhuri au ulipaji wa tozo mbalimbali ufanyike kwa njia ya kielektroniki. Lakini mtakumbuka kulikuwa na malalamiko kutoka kwa madereva wa vyombo vya moto kuwa walikuwa wakibambikiziwa faini ya makosa ya usalama barabarani ambayo hawakutenda," alisema Misime.

"Malalamiko mengine yaliyokuwa yakitolewa na madereva kwamba namba ya gari iliyoandikwa katika risiti ya faini ni gari anaoendesha, lakini namba ya leseni ya udereva si yake. Changamoto na malalamiko hayo yanakwenda kutatuliwa na mashine hizi mpya kutokana na uwezo wake kidijitali wa kuchukua kumbukumbu mbalimbali."

Kwa muhjibu wa jeshi hilo, mashine hizo zitazinduliwa hivi karibuni na zitajulikana kwa jina la Android Poss Mashine.

Alisema mashine hizo zitakuwa na uwezo wa kuruhusu kuingiza kumbukumbu tofauti na zile za awali pamoja na kuchukua alama za vidole.

"Hivyo ikitokea dereva anaandikiwa faini atachukuliwa pia alama za vidole na mashine hiyo," alisema Misime.

Alisema mashine hizo pia zina uwezo wa kupiga picha leseni na namba ya gari, kuhifadhi kumbukumbu kwa ajili ya rejea ya baadae, itakuwa na orodha ya makosa yote 37 ya usalama barabarani na itatumika katika kulipia maduhuri mbalimbali ya serikali ikiwamo taarifa za kupotelewa (loss report), kulipia silaha, na ukaguzi wa gari.

Pia alisema itatumika katika eneo lolote kutokana na uwezo wake wa kutumia mtandao wa kampuni ya simu zaidi ya moja.

"Ina uwezo wa kutumia mtandao wa kampuni ya simu zaidi ya moja na pia kutumia WiFi, na kasi yake ya mtandao ni ya 4G tofauti na poss ya awali iliyokuwa na spidi ya 2G," alisema Misime.

Mbali na hayo, itakuwa na uwezo wa kusoma taarifa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikiwamo kuunganisha kumbukumbu za leseni ya udereva au namba ya gari na jina kamili.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunataka Spika atakayesimamia majukumu ya Watanzania

**WIKI** hii ndiyo uamuzi wa majina matatu yatakayopelekwa kwenye kikao cha wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya kupigiwa kura ikiwa ni baada ya kumalizika mchujo ngazi ya Sekretarieti na Kamati Kuu ya CCM.

Ndani ya chama hicho jumla ya makada 70 ambao baadhi wamewahi kuwa au ni viongozi hadi sasa katika nafasi mbalimbali, walijitokeza kuomba ridhaa ya chama chao kugombea kiti cha Spika wa Bunge. Kati ya vyama vya siasa 22 vilivyoko nchini kwa sasa, ni ADC pekee ndiyo kimesimamisha mgombea, Maimuna Kassim.

Mkutano wa sita wa Bunge la 12, utafanyika kuanzia Februari mosi hadi 11, mwaka huu, ukijumuisha wabunge 392 ikiwa ni 263 wa majimbo, 113 viti maalum, watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wabunge wa Kuteuliwa na Rais 10. Hadi sasa mchuano mkali uko ndani ya CCM kwa kuwa kina wabunge 363, ikiwa ni 213 wa majimbo, Viti Maalum Bara na Visiwani 112, wa kuteuliwa tisa, hivyo kwa wingi wa kura spika atatokana na chama hicho.

Kwa mujibu wa kitabu cha orodha ya wabunge kilichoko kwenye tovuti ya Bunge, wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni 20 kati yake mmoja wa jimbo na 19 Viti Maalum.

Aidha, ACT-Wazalendo kina wabunge wa majimbo wanne na Chama cha Wananchi (CUF) kina wabunge watatu.

Watanzania wana matarajio makubwa kwa Spika atakayepatikana kuongoza muhimili huo utoe sura ya uwakilishi wa wananchi wa kawaida ambao walishiriki kupiga kura kwenye uchaguzi wa 2020.

Kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Tanzania inasema, Bunge litakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Muungano pamoja na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake.

Katiba ambayo ndiyo sheria mama inalitaja Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge linawenza kumuuliza waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma.

Pia kujadili utekelezaji wa kila wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti, kujadili na kuridhia mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudia kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.


Mjukumu mengine ni kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo, kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu nchi ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Tunataraji spika atakayepatikana ataweka kipaumbele kwenye kusimamia majukumu yake ili tuone uwakilishi wa wananchi kwenye chombo hicho. Tupo kwenye ulimwengu wa kidigitali ambao wananchi wanapata taarifa kwa haraka zaidi, wanahitaji kujua wanachojadili, yanayopitishwa na uwajibikaji wa chombo chao, hivyo lazima tupate spika anayejua mabadiliko yaliyoko duniani na mahitaji ya wananchi kwa sasa.

Tunapokumbuka maspika waliopita hasa wakati wa mfumo wa vyama vingi Bunge linalokumbukwa ni la Tisa lililoongozwa na marehemu Samuel Sitta, ambalo lilijulikana kama Bunge la speed (kasi) and standard viwango. Katika Bunge hilo tuliona wabunge wakihoji serikali mambo ya msingi yanayogusa maisha ya watu, kushughulikia rushwa ikiwamo kuunda kamati ya kuchunguza sakata la rushwa ambalo lilipelekea baadhi ya viongozi kuwajibika.

Tunaamini spika akiwa imara, mwadilifu na mwajibikaji tutakuwa na Bunge imara ambalo litafuatilia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za serikali pamoja na kutunga sheria zinazoendana na wakati wa sasa na uhalisia wa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani 'traffic light' mpya Dar safi, ila kuna shida ratiba ya dakika zake

**KUKUA** kwa teknolojia kumerahisisha huduma mbalimbali kwenye jamii, ikiwamo miundombinu ya barabara, ambako sasa taa za kuongoza magari maarufu 'traffic light' hivi sasa ni za kidigitali, jijini Dar es Salaam, kukipendeza hasa.

Matumizi ya huduma kidigitali yameleta mapinduzi makubwa kiuchumi ikiwamo kuokoa muda, kwa sababu huduma zinapatikana papo hapo na si analogia ambao ulikula muda wa watu wengi.

Hiyo inamaanisha kwamba imeirahisishia hata polisi usalama barabarani, kulazimika kukaa kwenye kila makutano ya barabara penye askari wa kuongoza magari tena kwa kupokezana, mfano halisi ni awali eneo la Ubungo.

Makutano hayo ya Ubungo kabla ya kujengwa daraja la juu liitwalo Kijazi, foleni ilikuwa kubwa na kusababisha usumbufu kwa watumiaji. Iliwachukua muda mrefu eneo hilo hata zaidi ya saa nne hadi tano kuvuka. Leo hii ni hadithi ya zama za kale.

Sasa, kuwapo kwa taa za kisasa za kidigitali zinazotumia sekunde kutokana na 'zilivyosetiwa' kumefanya foleni iwe historia kwa kuwa muda unaonekana wazi na kumwandaa dereva kuondoka kwa muda sahihi, ingawa changamoto imeanza kujitokeza tena eneo hili.

Majira ya jioni taa zinazoongoza magari hasa yanayotokea eneo la Mwenge kuelekea maeneo tofauti, ikiwamo Kimara, Buguruni, kutokana na hali iliyopo kwamba muda wa taa nyekundu 'kusetiwa' sekunde nyingi kuliko muda wa taa za kijani inayoruhusu magari kuondoka, ambayo ni sekunde 30.

Hivi sasa muda wa kuruhusu magari ni sekunde 120 au dakika mbili, ambazo kutokana na wingi wa magari hayo kutoka upande mmoja kuelekea nje ya mji kuwa mengi majira ya jioni.

Kuwekwa sekunde za kuruhusu magari kuondoka kuwa mdogo (sekunde 30) kuliko ule wa kusubiri (sekunde 120), pengine wataalamu wa masuala ya barabarani wana majibu, ingawa ukweli ni kwamba foleni katika daraja hili inaanza kurudi kimya kimya.

Kutokana na hilo, ni vyema mamlaka husika zikafuatilia suala hili na kubaini muda sahihi ambao unahitajika eneo fulani hususani katika makutano ya barabara zote jijini, kwa kuwa ukweli kwamba majira ya asubuhi mtiririko wa magari kutoka nje ya mji kuja mjini kati ni mkubwa.

Vivyo hivyo majira ya jioni magari yana kuwa na mtiririko mkubwa kutoka mjini kati kuelekea nje ya mji, hivyo kuliko na taa za kuongozea magari barabarani muda 'usetiwe' ambao unaoendana na majira husika.

Hilo linawezekana, kwa sababu hivi sasa taa zilizofungwa jijini sehemu nyingi ni za kidigali ambazo 'zinasetiwa' na hii itasaidia kupunguza usumbufu na kuondoa foleni pasipo sababu.

Suala la taa hizo kuchukua muda mrefu upande mmoja bila ya kuzingatia majira, inaathiri maeneo mengine kama vile taa za kuongoza magari yanayoingia na kutoka njiapanda ya ITV.

Majira wa jioni mtu akifika kwenye njiapanda ya ITV, mtiririko mkubwa wa magari huwa ni kutoka njiapanda hiyo na kuingia barabara ya Bagamoyo, kipaumbele kwa magari yanayotokea ITV kuliko eneo la viwanda na shughuli nyingine, ni kidogo.

Hali hiyo, pia inaleta foleni kubwa eneo la njiapanda, kutokana na taa hizo kupewa kipaumbele kikubwa kwa magari pekee yanayotoka na kueleke mjini kati.

Hili, wataalamu waliangalie na kulifanyia kazi, mtu akisimama maeneo haya machache ya yaliyotajwa kwa mfano, atabaini kitu kwamba aidha foleni inasababishwa na taa nyekundu au ya kijani katika makutano ya barabara.

Wakati teknolojia inakuja kurahisisha huduma na shughuli mbalimbali, iwe ukombozi wa kubadili fikra na mitazamo kwamba 'kupoteza muda hata wa nusu saa si kitu' ni mazoea au utamaduni wetu.



Kanisa la EAGT la Temeke, mkoani Dar es Salaam, likiwa limeanguka upande mmoja, baada ya kubomolewa hivi karibuni kutokana na mgogoro wa umiliki wa ardhi kati ya kanisa hilo na familia ya marehemu John Mfuko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waeleza mafanikio ya kuwapanga machinga

**Na Salome Mwasamale**

MIEZI miwili baada ya kufanyika kwa zoezi la kuondoa wamachinga walioko pembezoni mwa barabara, wafanyabiashara jijini Dar es Salaam wamepongeza zoezi hilo na kudai kuwa limepandisha thamani ya fremu za maduka na kuongeza pato la Taifa kwa kuwa wanalipa mapato yao serikalini bila shida.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wafanyabiashara walisema licha ya kuwa zoezi hilo limewaumiza baadhi ya watu waliokuwa wakifanya biashara zao pembezoni mwa barabara, lakini lina tija ya kutosha kwa manufaa ya nchi.Mo Nurdin, mfanyabiashara wa viazi Chanika mkoani Dar es Salaam alimpongeza Rais Samia Hassan Suluhu kwa nia yake njema ya kuongeza pato la taifa kwa kusababisha wanunuzi kufika madukani moja kwa moja na kujipatia bidhaa zao, hali ambayo inatoa fursa kwa wafanyabiashara kulipa ushuru serikalini bila shida. Nurdin alisema awali kulikuwa na changamoto kubwa ya ulipaji kodi kutokana na wafanyabiashara kuzuiwa biashara zao na wengine waliyopo mbele yao, huku wakilipa gharama ndogo ya Sh. 20 kwa mwaka tofauti na wao ambao hulipa karibu Sh. milioni 4 kwa mwaka. "Kwa kweli sisi wafanyabiashara wa maduka tunampongeza sana mama (Samia) kwa ujasiri huu na maamuzi haya magumu, lakini yenye tija ambayo tunaamini moja ya sababu zilizosababisha kuwapo kwa zoezi hili ni kuondoa migogoro ya mara kwa mara iliyopo kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na sisi wafanyabiashara," alisema.

Naye Philipo Rali na Onesmo Masawe walilipongeza zoezi hilo kwa madai kuwa limepunguza ajali nyingi za barabarani pamoja na kuifanya mitaro ya maji machafu iliyopo pembezoni mwa barabara kutoziba na kuufanya mji kuwa safi. Renatus Mroso, dereva bodaboda kituo cha Sonata kilichopo Chanika, Dar es Salaam alisema zoezi la kuwaondoa wamachinga pembezoni mwa barabara kumewanufaisha wengi na siyo wafanyabiashara wa maduka pekee.

Mroso alisema zoezi hilo limewanufaisha pia waendesha bodaboda kwa kuwa sasa wanaonekana kwa haraka na abiria na wanafanya kazi zao kwa ufanisi.

# Jela miaka tisa kwa kubaka mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete kisiwani Pemba, imemhukumu kijana Ali Juma Said, mkazi wa shehia ya Utaani kwenda jela miaka tisa na kulipa fidia ya shilingi milioni moja, baada ya kupatikana na kosa la kutorosha na kubaka binti wa miaka 14.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Wete, Abdallah Yahya Shamhun, baada ya kuona ushahidi uliotolewa mbele ya mahakama hiyo kutoacha shaka yoyote.

Hakimu huyo alisema baada ya kupatikana kwa ushahidi, mshtakiwa alionekana ni mkosaji na kumhukumu kutumikia adhabu hiyo.

"Mshtakiwa utakwenda kutumikia chuo cha mafunzo miaka miwili kwa kosa la kutorosha na miaka saba kwa kosa la kubaka na adhabu hizo zitakwenda sambamba," alisema.

Awali, wakili wa serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Juma Mussa Omar, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia kama hiyo.

Mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Desemba 30, mwaka 2020, alimtorosha mtoto huyo na kumpeleka nyumbani kwake Utaani na kumbaka.

Kubaka ni kosa kinyume na kifungu cha 108(1), (3), (d), na 109 (1) sheria ya adhabu, sheria nambari 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

# Wataka polisi kuongeza doria kuwadhibiti wezi

**Na Salome Mwasamale**

JESHI la Polisi limeombwa kuimarisha ulinzi na usalama hasa maeneo ya pembezoni mwa miji kwa kuwa matukio ya wizi yameongezeka.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baadhi ya wananchi walisema wizi sasa umeshamiri, hali inayowafanya wananchi kuchoshwa na kadhia hiyo na kujichukulia sheria mikononi.

Mayasa Dienga mkazi wa Kibuta Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, alisema wizi sasa umeongezeka mno hali ambayo inakatisha tamaa kwa kuwa watu wanahofia kutoka majumbani wakihofia kuibiwa.

Samwel Msenga, mkazi wa Kinyerezi mkoani Dar es Salaam, alisema zamani walizoea kuona doria za mara kwa mara zikifanywa na Jeshi la Polisi, lakini sasa zimepungua.

"Jeshi la Polisi liongeze doria, hali sasa ni mbaya na wananchi wamechoshwa na hali hiyo, ndio maana sasa wanachukua sheria mikononi za kuwachoma moto wahalifu wanapowakamata," alisema.

Naye Ramadhani Asukile mkazi wa Chanika, Dar es Salaam, alisema wezi sasa hawatafumbiwa macho kwa kuwa wanarudisha watu nyuma kimaendeleo kwa kuiba mfululizo bila kujali usiku au mchana.

Alisema wezi sasa huingia kwenye nyumba za watu na kuamua kula hadi chakula kisha kubeba vyombo na kuondoka, hali ambayo inaonyesha kuwa wana uhakika hawatakamatwa.

"Najiuliza sijui wanajivunia nini hawa wezi tunaliomba Jeshi la Polisi liongeze ulinzi amani imetoweka mitaani," alisema.

# Wadau wa maendeleo waridhishwa na TASAF

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na wadau wa maendeleo wamekutana kufanya mapitio ya kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamaga, alifungua kikao hicho jijini Dar es Salaam, jana kilichohudhuriwa na wadau wanaochangia utekelezaji wa mpango wa TASAF ikiwamo Benki ya Dunia, mashirika ya umoja wa mataifa ya ILO, WFP na UNICEF.

Wengine ni wawakilishi kutoka SIDA, Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Ubalozi wa Uswisi, Ubalozi wa Norway, Bill and Melinda Gates Foundation na FSDT, wawakilishi kutoka halmashauri za Kagera, Magu, Chunya na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

Mwenyekiti Mwenza wa kikao hicho ambaye pia ni Kiongozi wa Shughuli za TASAF katika Benki ya Dunia nchini Tanzania, Michele Zini, aliipongeza TASAF kwa kazi ya kupitia miradi ya ajira za muda, kujenga uchumi wa kaya na uhawilishaji Fedha.

Alisema Benki ya Dunia pamoja na wadau wengine wanaochangia TASAF wameridhishwa na utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu na wanajivunia mafanikio ya walengwa ambao wamepiga hatua katika kujikwamua kiuchumi na kuwapatia watoto wao mahitaji yao ya msingi.

Alisema wakati wa vikao vya mapitio, washiriki hutembelea maeneo ya utekelezaji na kufanya mazungumzo na walengwa, watendaji na viongozi. Hata hivyo, katika kipindi hiki, ziara hazitafanyika na badala yake wawakilishi watatoa taarifa za utekelezaji wa maeneo yao.

Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa TASAF utahusisha kujadili taarifa za utekelezaji, kubainisha changamoto za utekelezaji na hatimaye kuja na mapendekezo ya kuboresha kipindi kilichobaki na kitakachofuata.

Zini alisema kipindi cha pili cha Mfuko wa TASAF kilipozinduliwa, kulitokea matukio mengi yaliyosababisha kuchelewa kuanza kwa utekelezaji, lakini kazi zote zilizopangwa zilifanyika kwa ufanisi ikiwamo walengwa wa zamani kuhakikiwa, wapya kutambuliwa na kulipwa stahili zao ndani ya dirisha la malipo lililofunguliwa mwezi Januari 2022.

Alisema kaya za walengwa wa kipindi cha kwanza walilipwa malipo yao kwa mikupuo miwili. Wapya na kipindi cha pili walilipwa mkupuo mmoja wa kwanza na fedha iliyolipwa ni Sh. bilioni 51.1.

Jumla ya miradi 3,185 imeibuliwa na inatarajiwa kutoa ajira kwa walengwa 195,000 ambao watalipwa jumla ya Sh. bilioni 36 kama ujira wa kushiriki katika kazi hizo kwa mwaka 2021-2022 katika vijiji, mitaa, shehia 2,349 za Tanzania Bara na Zanzibar.

"Lengo la mapitio ya kipindi cha pili cha Mpango wa TASAF ni kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji na kujadili namna bora ya kukamilisha kipindi hiki ambacho kinatarajiwa kukamilika 2023," alisema Zini.

Vile vile, amegusia uwezekano wa kuongeza muda wa utekelezaji wa kipindi hicho cha pili ili kukamilisha mipango iliyowekwa.

# Watahadharishwa uchimbaji wakati wa mvua

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga wametakiwa kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua ili kuepuka ajali za kuangukiwa na kifusi cha udongo wanapofanya uchimbaji.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana mjini hapa na Ofisa Madini Mkazi wa mkoa wa kimadini Kahama, Jeremiah Hango alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake. Hango alikuwa akitoa taarifa kwa wachimbaji wadogo kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na majanga yanayojitokeza kipindi cha mvua.

Alisema kipindi cha mvua mashimo ya wachimbaji wa madini yanajaa maji na kukosa uimara na wakati mwingine hutitia na kusababisha maafa kwa wachimbaji wadogo na ili kuondokana na tatizo hilo aliwataka kuendelea kuchukua tahadhari kabla madhara hayajatokea.

Hango alisema kabla ya kuingia shimoni na kuendelea na shughuli za uchimbaji ni vyema wakakagua kama kuna maji ndani na kuyaondoa.

Alisema hatua hiyo itawasaidia kupata nafasi ya kufunga magogo ambayo yanazuia udongo au shimo kutitia hali itakayowafanya kuwa salama kipindi chote cha uchimbaji.

"Watabiri wa hali ya hewa wanadai kutakuwa na mvua kubwa na upepo mkali kwenye mikoa 10 Kanda ya Ziwa ambayo itasababisha mashimo kujaa maji kupita kiasi, hakikisheni mnakagua kama kuna maji na kuyaondoa na fungeni magogo imara yatakayozuia shimo kutitia na sio kufika na kuingia shimoni," alisema Hango. Aliwataka wenyeviti wa migodi midogo kujenga desturi ya kukagua maduara ya wachimbaji wadogo kabla ya kuwaruhusu kuendelea na shughuli za uchimbaji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha wachimbaji wadogo wa madini mkoani Shinyanga, Hamza Tandiko, alisema kwa sasa wanaendelea na kampeni ya utoaji wa elimu kwa wachimbaji hao ili kulinda maisha yao mahala pa kazi.

Alisema kampeni hiyo inakwenda sambamba na utoaji wa elimu ya UVIKO-19 na chanjo yake ili kuhakikisha wachimbaji wote wanachanjwa kulinda afya zao na kuwakinga wenzao.




Mshindi wa promosheni ya Vodacom "Show Love, Tule Shangwe", Neema Rajabu (wa pili kulia) kutoka Chato, akiwa na zawadi zake za televisheni za kisasa, baada kukabidhiwa na kampuni ya Vodacom Tanzania, katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya stendi ya Igombe, jijini Mwanza mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapongeza hatua ya kushughulikia bidhaa kupandishwa bei kiholela

**Na Daniel Limbe, CHATO**

BAADHI ya wananchi wilayani Chato, mkoani Geita wamempongeza Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji kwa kuagiza Tume ya Ushindani Nchini (FCC), kumpatia taarifa za sababu za kupanda bei vinywaji baridi pamoja na vifaa vya ujenzi bila utaratibu.

Licha ya wananchi hao kudai agizo hilo kuchelewa, walisema litasaidia kuwabaini wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi wanaopandisha bei kiholela kwa lengo la kujipatia faida kubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule, hivi karibuni alikumbana na kadhia ya kupanda vifaa vya ujenzi wakati akikagua miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya na vyumba vya madarasa ya sekondari.

Tusila Simeo, mhudumu wa afya katika Zahanati ya Katende, alisema ujenzi wa kituo cha afya unaweza kugharimu fedha nyingi kutokana na kupanda kwa vifaa vya ujenzi.

Alitoa mfano kuwa kwa sasa mfuko mmoja wa saruji unauzwa Sh. 23,000 ikilinganishwa na awali ulipouzwa Sh. 20,000, nondo kutoka Sh. 22,000 hadi Sh. 27,000 huku vigae vikipanda kutoka Sh. 24,000 hadi Sh. 28,000. Kwa upande wake, wakala wa saruji mjini Chato, Daud Machafu, akizungumzia hali ya kupanda vifaa hivyo alisema, kunatokana na uzalishaji mdogo wa viwanda vya ndani ikilinganishwa na mahitaji.

Vile vile, alisema gharama kubwa za usafirishaji zinachangia kupanda kwa bei na kwamba wafanyabiashara hawana namna ya kuzishusha.

Mmoja wa wananchi wilayani Chato, Christina John, aliomba kudhibitiwa mfumuko wa bei sokoni ili kunusuru uchumi wa wananchi hususani waliopo vijijini.

# WAJIKI yajitosa kampeni chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), linalojishughulisha na kampeni ya kupinga rushwa ya ngono kwa wanafunzi, limeongeza kampeni nyingine ya kuhamasisha umma kupata chanjo ya UVIKO-19.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa shirika hilo, Janeth Mawinza, alisema kampeni hiyo inafanywa na madereva wa bodaboda, bajaj na daladala ambao ni wanachama wa WAJIKI.

"Kwa sasa tunatengeneza barakoa, vitakasa mikono, ubuyu na sabuni vikiwa na ujumbe wa 'Jikinge na corona pambana na rushwa ya ngono', hivyo tunaunga mkono vita hii ya kutokomeza corona," alisema Janeth.

Alisema, baadhi ya madereva wa bodaboda, bajaj na daladala, katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke, ni mabalozi wa WAJIKI, wanahamasisha jamii kuepuka rushwa ya ngono, ambapo sasa wameongeza kazi nyingine ya kuhamasisha kampeni ya chanjo.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mabalozi hao wa WAJIKI wana vikundi 108 vyenye madereva 3,741 katika wilaya hizo tatu wakipiga kampeni ya kupinga rushwa hiyo na pia kuhimiza umuhimu wa kupata chanjo.

Janeth alisema, shirika lake kwa ufadhili wa Taasisi ya Women Fund Tanzania Trust (WFT), linapiga vita rushwa ya ngono, na kwamba limeamua kuunga mkono serikali katika mapambano ya UVIKO-19.

Alisema, shirika lake kutengeneza barakoa, vitakasa mikono, ubuyu na sabuni na kuweka maandishi yanayohamasisha watu kujikinga na ugonjwa huo, inaonyesha jinsi ambavyo liko mstari wa mbele kupambana na ugonjwa huo.

"Hivyo, kampeni yetu ya 'Safari Salama kwa Wasichana na Wanafunzi bila Rushwa ya Ngono Inawezekana' inaendelea katika vijiwe mbalimbali vya madereva hao huku wakipenyeza nyingine ya kujikinga na corona," alisema. Kuhusu rushwa ya ngono, alisema inaendelea kuumiza jamii kimya kimya, kwa kuwa kitendo hicho kinafanywa kati ya watu wawili kwa siri kubwa, lakini madhara yake yanabaki kuwa ya muda mrefu kwa aliyeombwa rushwa hiyo.

Ikumbukwe kuwa madereva hao ndiyo wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na rushwa hiyo, ndiyo maana tukaamua kuwashirikisha katika vita hii, kwani wanapomtamani mwanafunzi hutumia nyenzo waliyonayo kuwasafirisha kwa malengo ya kuwalaghai na kupata rushwa ya ngono," alisema.

Janeth alisema, inasikitisha kuona watu wanaotakiwa kuwapa wanafunzi huduma ya usafiri, ndiyo ambao huwaomba rushwa ya ngono na mwisho wa siku wanawaachia madhara ya kiafya.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Dk. Elirehema Doriye (kulia), Mkurugenzi wa Masoko na Huduma kwa Wateja NIC, Yessaya Mwakifulefule (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Karimu Meshack, wakiangalia Soko la Karume, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kuteketea kwa moto, walipotembelea kwa ajili ya kutoa pole kwa wafanyabiashara na serikali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walia utitiri tozo mfumo stakabadhi ghalani

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WAKAZI wa Kijiji cha Mchuruja Kata ya Tuwemacho wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamelalamikia utitiri wa tozo kwenye mazao yao wanapouza kwenye masoko ya mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani.

Kwa mujibu wa wakulima hao, takribani shilingi 288 zinatozwa kwenye kila kilo moja ya korosho inayouzwa sokoni kupitia mfumo huo.

Rameck Mtuya ni miongoni mwa wananchi waliopaza sauti zao kwa kulalamikia tozo hizo mbele ya Mbunge wa Tunduru Kusini, Daimu Idd Mpakate, ambaye alifanya ziara ya kuwashukuru wananchi wa kata hiyo kwa kumpatia ridhaa ya kuwaongoza katika kipindi cha 2020/2025.

Mtuya alisema makato hayo ni makubwa mno ukilinganisha na kipato cha mkulima ambaye kilimo hicho ndiyo tegemeo lake la kujikwamua kimaisha.

Pia walitoa kilio kuhusiana na zao la mbaazi kwamba kwa kuwa hata wabunge walisema zao hilo ni mboga na hata yakiuzwa kiasi fedha zake hubakia kuwa matumizi nyumbani, hivyo kupinga kuliuza kupitia mfumo huo kwa maelezo kiwa kufanya hivyo ni usumbufu.

"Tunajitahidi kulima mazao mbalimbali ikiwamo mbaazi ambalo katika msimu wa mwaka 2020/2021 tuliuza kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, lakini cha kushangaza hadi sasa wapo baadhi ya wakulima ambao hawajalipwa," alisisitiza Mtuya na kuiomba serikali kufanya mabadiliko.

Alimwomba mbunge huyo kupeleka serikalini maombi ya kuruhusiwa kuuza mbaazi zao kupitia mfumo wa soko huria.

Akijibu kero hizo, Mbunge Mpakate alikiri kuwapo kwa tatizo na kwamba kuna mambo ambayo kwa sasa wabunge wanaishauri serikali likiwamo suala la kuichangia Bodi ya Korosho shilingi 25 kwenye kila kilo moja inayouzwa sokoni.

Alisema sheria ya mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani ulipitishwa na Bunge mwaka 2009 baada ya kuonekana kuwa na manufaa makubwa kwa wakulima ikilinganishwa na mfumo wa wakulima kuuza mazao holela.

Kuhusu makato yanayo lalamikiwa na wananchi wake, alisema yapo makato ya kisheria ambayo wajumbe wa tasnia ya mazao mchanganyiko walikubaliana kwenye vikao vyote.

Alisema anachokiona yeye ni watendaji wanaosimamia mfumo huo kutotimiza maelekezo ya kuweka wazi kwa kubandika kwenye mbao za matangazo makato ambayo walikubaliana ili wakulima wayajue wanapoenda kuuza mazao ghalani.

## Wapewa siku 13 kutatua mgogoro kwenye mgodi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, ametoa siku 13 kwa uongozi wa Wilaya ya Iramba na Ofisi ya Madini Mkoa wa Singida kumaliza mgogoro ulioko kwenye kitalu namba 22 unaosababishwa na wanachama na wadhamini wa mgodi wa Ukombozi, kutokana na mgongano wa kimaslahi.

Dk. Kiruswa alitoa maagizo hayo juzi wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa mgodi wa Ukombozi katika ziara yake ya siku moja ya kujitambulisha na kujionea baadhi ya miradi inayotekelezwa na wizara hiyo hasa katika sekta ya madini na kujua changamoto za wachimbaji.

Dk. Kiruswa baada ya kusikiliza malalamiko ya pande zote mbili alisisitiza kuwa kama pande hizo hazitafikia makubaliano, serikali inaweza kufuta leseni hiyo na kutoa kwa mwekezaji mwingine ili uzalishaji uweze kuendelea.

"Natoa siku 13 kwa uongozi wa Wilaya ya Iramba na Ofisi ya Madini Mkoa wa Singida kumaliza mgogoro uliopo kwenye kitalu hicho katika machimbo ya Ukombozi, vinginevyo serikali inaweza kuifuta leseni hiyo," alisema Kiruswa.

Katika hatua nyingine Kiruswa aliupongeza Mkoa wa Singida hasa watendaji wa sekta ya madini kwa kuvuka malengo ya ukusanya wa maduhuli kwa mwaka huu wa fedha, ambapo yalifikia asilimia 142.2 na kuwa hana shaka hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha mapato hayo yataongezeka kutokana na kufanya kazi vizuri.

Akijibu swali lililohusu wachimbaji wadogo kutopata leseni, alisema kazi kubwa ya wizara kwanza ni kuwatambua, kujua idadi yao na wangapi wanaleseni kwani malengo ya serikali ni kusimamia sekta ya madini huku dhamira ni kuona kila mchimbaji anapata leseni na vifaa kama walivyoomba.

Naye Kaimu Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Singida, Chone Malembo, akizungumzia sifa za mtu anayepaswa kupatiwa leseni ya uchimbaji, alisema sheria ya madini kifungu namba 8 kinaeleza anayeweza kupata leseni hiyo hata wachimbaji wadogo ili mradi awe ni Mtanzania mwenye umri isiyopungua miaka 18.

Alitaja sifa nyingine ni awe hajawahi kushtakiwa au kutangazwa na mahakama kama amewahi kufilisika.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Selemani Mwenda, alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/ 2021 waliweza kuzalisha gramu 319,000 na kuwa zimeweza kuiingizia fedha serikali Sh. bilioni 37, ambapo mapato yaliyotokana na madini yalikuwa ni zaidi ya Sh. bilioni 400.

# Mfuko wa jimbo kulikarabati soko

**Na Happy Severine,** MASWA

MBUNGE wa Maswa Mashariki mkoani Simiyu, Stanslaus Nyongo, amesema kiasi cha Sh. milioni 42 za mfuko wa jimbo hilo zitatumika katika ukarabati wa miundombinu ya soko mjini Maswa.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa kikao cha kamati ya maendeleo ya mfuko huo kilichofanyika mjini Maswa, alisema kuwa wajumbe wote wa kamati hiyo wameridhia kutumika kwa fedha hiyo.

Nyongo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Mfuko wa jimbo hilo, alisema kukarabatiwa kwa soko hilo itakuwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa kwa wananchi wa mji huo baada ya kutembelea soko hilo na kuona ubovu wa miundombinu inayosababisha kero kwa watumiaji wa soko hilo pamoja na wafanyabiashara hasa nyakati za mvua. Alisema nyakati za mvua maji hujaa ndani ya soko hilo na kusababisha tope, hivyo kuwa kero kwa watu wanaofika katika soko hilo kupata mahitaji mbalimbali.

"Soko hili ni la muda mrefu limejengwa wakati tunapata Uhuru na tangu kipindi hicho halijawahi kukarabatiwa ndiyo maana unaona miundombinu yake kwa kweli imechakaa sana," alifafanua.

"Kwa nyakati za masika mvua zinaponyesha huwa ni kero humu ndani ya soko, maana maji yanajaa na tope linakuwa jingi, hivyo kusababisha kero kwa wafanyabiashara na watu wanaoingia kutafuta mahitaji," alisema. Aliongeza kuwa wataanza kuweka vigae vya tofali chini pamoja na sakafu ili kudhibiti tope ndani ya soko hilo sambamba na kuhakikisha maji yatakayoingia yanatoka kupitia mitaro ya maji itakayowekwa.

Nyongo alisema kiasi cha fedha kilichotengwa iwapo hakitakidhi ukarabati huo, watatumia fedha nyingine za mfuko wa jimbo kuhakikisha soko hilo linakuwa katika hali nzuri ili wafanyabiashara na wananchi wanaofika kununua mahitaji wanakuwa katika mazingira mazuri.

Aidha, alisema mipango ya baadaye ni ujenzi wa soko jipya la kisasa, ili liendane na hali ya sasa ya mji huo, na kwamba tayari ameshaanza mazungumzo na Balozi wa Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE) nchini ili kupata fedha za ujenzi huo.

Naye Katibu wa soko hilo, Naftari Yoram, alisema kwa hatua hiyo ya awali ya ukarabati huo, itawasaidia kupunguza kero ya tope ndani ya soko hilo, huku akiiomba serikali nayo kuunga mkono jitihada za mbunge huyo ili waweze kujenga vibanda vya kisasa tofauti na hali ya sasa ya vibanda vya mabati vyenye mapaa yanayovujisha maji nyakati za mvua.



Rundo la takataka likiwa limetelekezwa bila ya kuzolewa katika Mtaa wa Mapinduzi, Kata ya Ndala, Manispaa ya Shinyanga jana na kutishia usalama wa afya za wananchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Walia uchafu kuzagaa makazi ya watu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga, wameomba serikali kuondoa uchafu uliorundikana jirani na makazi yao kwa muda mrefu na kuhatarisha afya zao.

Walibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, wakati akizungumza na wananchi mbalimbali zikiwamo kaya maskini.

Mkutano huo ulifanyika katika mtaa wa Mapinduzi, Kata ya Ndala.Mmoja wa wananchi hao, Rehema Mussa, alisema ghuba la kuhifadhi uchafu limejaa na kusababisha kuanza kuzagaa pembeni.

Aliomba serikali kuondoa uchafu huo ambao umekuwa ukitoa harufu mbaya pamoja na kutishia afya za wananchi wanaoishi jirani na eneo hilo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mapinduzi, Zabibu Cosmas, alisema ghuba hilo limekuwa likikaa zaidi ya miezi mitatu bila ya kuzolewa uchafu na kutishia afya za wananchi.

"Mkuu wa Mkoa kwenye mtaa wangu huu wa Mapinduzi tuna kero kubwa ya ghuba la kuhifadhi uchafu kutozolewa kwa wakati na lipo jirani na makazi ya watu ambalo lina zaidi ya miezi mitatu halizolewi na uchafu umekuwa tishio kwa afya za wananchi," alisema Cosmas.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema katika manispaa yapo mengi ambayo hayazolewi kwa wakati.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Rajab Masanche, alisema tatizo lililosababisha taka kutozolewa kwa wakati kwenye ghuba ni kutokana na ubovu wa magari ya kuzolea.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, aliagiza halmashauri zote mkoani humo, kuweka wazabuni wenye uwezo wa kuzoa taka.

Aliagiza maeneo ya kukusanyia uchafu yasiwe jirani na makazi ya watu badala yake yawekwe mbali sehemu ambazo ni salama na hazihatarishi afya za wananchi..

# H'shauri Kibaha ilivyokamilisha ujenzi madarasa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani imekamilisha ujenzi wa vyumba 30 vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari.

Kukamilika kwa vyumba hivyo kutawezesha uwapo wa ongezeko la wanafunzi kutoka 7,275 hadi kufikia 8,690, jambo ambalo linaelezwa kuleta mabadiliko ya kielimu katika halmashauri hiyo.

Halmashauri hiyo imekuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa saba kwa upande wa sekondari, hali ambayo imekuwa ikisababisha wanafunzi kusoma wakiwa zaidi ya 50 katika chumba kimoja.

Katika taarifa ya Ofisa Elimu (sekondari), Fatuma Kisalazo, aliyoisoma kwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri jana, alisema kuwa ujenzi wa vyumba vya madarasa hayo umetokana na fedha za UVIKO-19.

Alisema kuwa halmashauri hiyo ilipokea Sh. milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 30 vya madarasa ambapo kati ya hivyo, 20 vya shule ya sekondari na 10 ni upande wa shule za msingi.

Alisema kuwa katika ujenzi huo pia wamefanikiwa kujenga shule mpya ambazo zitawezesha kupokea wanafunzi wa sekondari wa kidato cha kwanza na wale wa vidato vingine ambao awali walikuwa wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 10 kwa siku kufuata masomo kutokana umbali wa makazi na maeneo ya shule.

Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, aliwataka walimu na wanafunzi watakaoyatumia madawati pamoja na madarasa hayo kuyatunza ili yatumike kwa vizazi vilivyoko na vijavyo.

Akizungumza baada ya kupokea vyumba hivyo vya madarasa, Msafiri alionya kuwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi wilayani huko watakaobainika kuvunja madawati kwa makusudi, wazazi wao watawajibika kulipa kwa ajili ya gharama za mafundi watakaotengeneza.

ama
ALHAMISI JANUARI 20, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Simulizi maji tiririka yanavyobaki kuwa mkakati usio na makali vita Uviko – 19**


Ukurasa 14

**UKUAJI UBONGO WA MTOTO...**

**Mtaalamu aanika: Fikra, mantiki, uwezo kutafakari umejificha katika usomaji vitabu**

# Fahamu kinachozaliwa na kipigo kwa afya ya mtoto, matusi, pia unyanyasaji

- Nchini: Hofu ya aina mpya udhalilishaji
- UN: Tishio machafu yanayoibuka duniani
- Polisi na LHRC katika butwaa ya pamoja

**Na Rehema Gohage, SJMC**

MARA zote katika mjumuiko wa kijamii iwe kiimani, kijamii na hata kisheria mtoto hubaki kuwa mali ya umma na anatunzwa na huo umma, tafsiri inayokaa ndani ya mila, imani na sheria za umma kote duniani.

Ni ndani ya dhana hiyo, hivi karibuni katika mageuzi ya kimuundo; Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto imeundiwa wizara yake, ikiwa sehemu ya kuwapa umuhimu.

Mtoto anatafsiriwa kisheria kuwa mtu mwenye umri chini ya miaka 18, akiwa sehemu muhimu ya jamii na tegemeo endelevu kitaifa, hivyo inawapa umuhimu wa kulelewa vizuri na kuendelezwa.

Anna Henga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Tanzania, anautaja 'ukatili kwa watoto' ni kitendo kinacholenga kumdhuru au kumsababishia maumivu mtoto, mfano ni ubakaji, vipigo na kuwatelekeza.

Watoto hao wana mahitaji na anayewajibika nayo ni mzazi na jamii kwa upana, ikiwamo afya na elimu, kumuandaa kuwa mshiriki wa baadaye wa maendeleo ya dunia nzima.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga. **PICHA: MTANDAO.**

Sheria ya Mtoto inalenga kuimarisha ulinzi, matunzo na haki zake, zikiwamo kulelewa na wazazi, mahitaji ya msingi kama chakula, malazi, mavazi, matibabu, chanjo, elimu, kucheza na kuburudika.

**JICHO LA UMOJA MATAIFA**

Ripoti ya Umoja wa Mataifa Juni mwaka jana, inatahadharisha nchi zimeshindwa kuzuia ukatili kwa watoto, ikitoa wito wa kuchukuliwa hatua za kuzuia athari kubwa zaidi.

Ripoti ya pamoja ya Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhudumia Watoto (UNICEF), pia Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO), zinadadavua kwa kina ukatili dhidi ya watoto duniani .

Zinataja kimataifa nusu yao duniani sawa na bilioni moja kila mwaka wanaathirika na ukatili wa kimwili, kingono au kisaikolojia, kujeruhiwa, kusababishiwa ulemavu na kifo na nchi zimeshindwa kuzingatia mikakati iliyowekwa kuwalinda.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO Dk. Tedros Adhanon Ghebreyesus, amesema "Hakuna uhuru wowote kwa ukatili dhidi ya Watoto. Tuna ushahidi wa nyenzo za kuzuia ukatili huo ambapo tunazitaka nchi zote kutekeleza, kulinda afya na ustawi wa watoto ni kiini cha kulinda afya yetu ya pamoja na ustawi wa sasa na siku za mbele."

Kwa jina 'Ripoti ya Hali ya Kimataifa Katika Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto 2020' ni ya kwanza ya aina yake, ikiainisha hatua za nchi 115 chini ya mkakati uitwao 'Inspire' uliogawanyika katika

**Inaendelea Uk. 12**

AFYA

# Fahamu kinachozaliwa na kipigo kwa afya ya mtoto, matusi, pia unyanyasaji



Watoto wakitandikwa viboko shuleni, sehemu ya adhabu zenye athari kwa afya ya mtoto. **PICHA: MTANDAO.**

Inatoka Uk. 11

mikakati saba ya kunusuru watoto na ukatili kwao.

Ripoti inabainisha haja ya nchi zote kuongeza juhudi kutekeleza mikakati hiyo na hadi sasa zinatajwa nchi nyingi (Asilimia 88 ya serikali zote) zina sheria muhimu za kuwalinda watoto dhidi ya ukatili, ingawa nusu yao tu ndio zinasimamia sheria hizo ipasavyo.

Ni mara ya kwanza, ripoti hiyo imejumuisha makadirio ya mauaji ya watoto hususani walio chini ya umri wa miaka 18. Zamani walijumuishwa kitakwimu na vijana umri kati ya miaka 18 na 19; jumla watoto wastani 40,000 waliuawa.

Chini ya robo za nchi tajwa zina mipango ya kubadilisha mila mbaya na asilimia 15 zimeshafanya mabadiliko kuwawekea mazingira salama watoto hao.

**RIPOTI NCHINI**

Nchini Tanzania, ripoti ya Jeshi la Polisi inaonyesha ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto. Mwaka 2020 kulikuwapo mikasa 7,388 ikilinganishwa na miaka mitano kabla, 2015 matukio 5,803. Ripoti hiyo inataja ukatili kwa watoto upo kiwango kikubwa kujumuisha dhuluma kingono, mwaka huo kukiripotiwa mikasa 7263 na ongezeko la asilimia 26, ikilinganishwa na mwaka 2015, kulirekodiwa matukio 5803. Huo ni wastani wa matukio 615 kwa mwezi, hali inayotajwa ni hatari kwa usalama wa watoto nchini.

Anna Henga, anafafanua ongezeko hilo kama zao la kushamiri imani za kishirikina ndani ya jamii wanaosaka utajiri, Kanda ya Ziwa kukitajwa ni vinara.

Ripoti zote zinataja ishara mbaya ya mwaka huo 2020, kumshamiri ukatili mpya wa watoto kubakana na kulawitiana shuleni; msingi na sekondari, vyombo vya habari vilihusika kuyaripoti kwa kiasi kikubwa.

Sophia Temba, Ofisa Programu Jukwaa la Utu wa Mtoto, anasema mmomonyoko wa maadili katika utandawazi, inachangia ongezeko la mabaya hayo, hata kuhitajika haja ya kutengwa bajeti toshelevu ya kuandaa mpango kazi kitaifa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto.

Mtaalamu Hawa Bihoga, katika andiko lake la Aprili 2021, anasema baadhi ya wazazi na walezi wanapaza sauti, pia ni ishara chanya ya kushamiri elimu kwenye jamii, kwani kabla ilikuwa jamii 'wakimalizana' wenyewe katika ngazi ya familia, wakihofia madhara ya sheria kuchukua mkondo wake.

Hata hivyo, anawakumbusha maofisa ustawi wa jamii, wana jukumu la kuhakikisha huduma ya ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya unyanyasaji, ukatili, utelekezaji na unyonyaji kisheria.

Hapo kuna suala la kupokea rufani za mashauri ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto, kuchunguza mahitaji ya mtoto na vihatarishi vinavyomzunguka na kuchukua hatua stahiki kisheria.

Pia, Hawa anataja jukumu la kuratibu na kusimamia uanzishaji kamati za ulinzi na usalama wa mtoto katika ngazi za halmashauri, kata na vijiji au mitaa, kujenga uwezo wa wazazi na walezi kuwapa watoto wao malezi bora, kutoa msaada kisaikolojia na kijamii kwa wahanga wa ukatili na unyanyasaji, mfano usafirishaji haramu wa binadamu, kuwapatia hifadhi ya muda wahanga wa ukatili na unyanyasaji watoto na wahanga wa usafirishaji haramu.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, anafafanua takwimu zilizopo kitaifa dhidi ya ukatili kwa watoto kulingana na taarifa ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2020, vinazidi kuongezeka zaidi, hasa kingono na kimwili.

Anashauri kwamba, si sahihi kumuadhibu mtoto kila anapokosea na adhabu zizingatie utu na usalama wake, ili zisimsababishie maumivu, bali kumfunza.

**MATUKIO YALIVYO**

Kuna matukio kadhaa yameripotiwa katika vyombo vya habari, yakieleza vitendo vya ukatili kwa watoto vilivyoweza kuleta matokeo hasi kwa watoto, mfano ni tukio la mkoani Tabora miezi mingi iliyopita baada ya mtoto kuuawa na jirani yake kwa shutuma za kumbaka mtoto wake wa kike.

Vilevile, tukio lililoripotiwa na Polisi jijini Dar es Salaam, mwanafunzi wa darasa la nne mwenye umri miaka tisa, kufariki kwa vipigo kutoka kwa mzazi mwaka jana.

Pia, Desemba iliyopita kushuhudiwa simulizi binti wa miaka mitano kunusuriwa na wasamaria kutoka mikono ya unyanyasaji kutoka kwa mama mlezi .

Naye, Humphrey Tito (jina sio halisi) mkazi wa jiji la Dar es Salaam anatoa kisa chake kuhusiana na adhabu ya viboko kutoka kwa mwalimu wake wa somo la hesabu, iliyotokea miaka mingi iliyopita iliyomsababishia maumivu makali na kujenga chuki ya kudumu kati yake na mwalimu huyo anayemfundisha.

Kanuni ya adhabu ya viboko inatumika panapotokea utovu mkubwa wa nidhamu au kosa kubwa ndani au nje ya shule ambalo litaishushia shule heshima.

Kanuni ndogo inafafanua adhabu ya viboko itolewe kwa kuzingatia umri, jinsia na afya ya mwanafunzi na isizidi viboko vinne kwa tukio lolote, tena ikiwa na kanuni za idhini yake chini ya mwalimu mkuu wa shule, sheria ikifafanua zaidi mwenye mamlaka ya kumchapa mwanafunzi.

Kanuni inaagiza kila adhabu ya viboko inapotolewa kwa mwanafunzi, kumbukumbu ya adhabu hiyo sharti iwekwe kwenye kitabu, ikitaja jina la mwanafunzi, kosa alilolifanya, idadi ya viboko na jina la mwalimu aliyetoa adhabu.

Sheria inataka uchunguzi na kujiridhisha kuwa mwanafunzi amehusika moja kwa moja na kosa analotuhumiwa nalo ndipo hatua ya kupeleka suala lake mbele ya mwalimu mkuu lifuate ili atumie mamlaka aliyopewa kisheria kutoa adhabu stahiki kwa mwanafunzi husika.

Je ni walimu wangapi wanaadhibu kwa mujibu wa sheria inayosimamia viboko, pia Sheria ya Watoto inayotawala nchini?

**WAZAZI vs ADHABU**

Mkazi wa jijini Dar es Salaam kutoka wilayani Kinondoni, Hassan Yassin, analalamikia vitendo vya ukatili kwa watoto hususani vipigo vilivyopita kiasi na lugha chafu inayoharibu malezi na kuchangia watoto kuwa waoga. Huku wengine wakiwa sugu wa adhabu wanazopewa.

Anna Henga, Mkurugenzi wa LHRC, ana maoni kwa adhabu rafiki kwa watoto ni zisizompa mateso au ukatili wa aina yoyote, bali kumfundisha na kumwelewesha kuelewa kosa, pia adhabu ziendane na umri wa mtoto.

Maria Joseph, mkazi wa Dar es Salaam, anaeleza sababu inayochangia wazazi kutumia lugha isiyo na maadili katika malezi na makuzi ya mtoto, ni ukosefu wa elimu ya athari za kisaikolojia mtoto anazokumbana nazo, pindi anapofanyiwa ukatili wa namna hiyo.

Henga anakumbusha kuwa, lugha chafu nayo inageukia katika ukatili chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Mtoto, 2009 wito wake walimu pamoja na wazazi au walezi waheshimu haki za watoto na kutambua haki zao.

AFYA

# Simulizi maji tiririka yanavyobaki kuwa mkakati usio na makali vita Uviko – 19

## •Mtendaji mwendokasi adai 'ugonjwa wa wakubwa'




Tangi la maji katika Stendi ya Mabasi Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, ilivyo hivi sasa. **PICHA: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika**

ILIKUWA siku ya 12 ya mwaka huu kuanzia, majira ya saa mbili na nusu asubuhi, niko katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam kwa ajili ya kutafuta usafiri wa kuelelekea kwenye shughuli zangu za kila siku.

Kabla ya kupanda daladala, nakumbuka misamiati na nadharia za maradhi Uviko 19 na tahadhari zake, ninaamua kuzunguka kidogo kituoni hapo kukagua namna abiria wanavyochukua hatua zinazoelekezwa na Wizara ya Afya, kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Katika 'zungukazunguka' Nipashe inatua hadi yanakoegeshwa mabasi ya Mwendokasi, kwa maana ya UDART, ikiwa kwenye moja ya vibanda vya kukatia tiketi ambako kuna tanki la kuhifadhi maji tiririka kwa ajili ya abiria kunawa.

Hata hivyo, kinachokutwa hapo ni tanki linaloonekana halijatumika kwa muda mrefu.Vumbi na hata eneo la chini yake ambako kunatakiwa kuwapo ndoo ya abiria wanaponawa yasimwagike, halipo.

Mazingira hayo yanasukuma kujisogeza hadi kwa wahudumu wa mabasi hayo kudadisi kwanini matanki hayo kituoni hayana maji na kuna hatua gani zinazochukuliwa kurekebisha huduma hiyo?

Penye moja ya mabasi ya mwendokasi yaliyoegeshwa kituoni hapo, anakutwa mmoja wa wahudumu wa mabasi nje ya mlango wa gari lake, akikagua tiketi za abiria wanaotaka kuingia ndani.

Akiwa na wajihi mnene kiasi, mweusi kidogo, nywele fupi zinazopendezeshwa na mvi kwa mbali, ndani ya shati nyeupe na suruali nyeusi, anaomba tiketi abiria wake.

Hapo kunagundulika jingine la ziada kuhusiana na corona katika foleni hiyo ya abiria wanaoingia, uvaaji barakoa umekosa nafasi, hali inayosukuma shauku ya udadisi kumhoji muhudumu huyo wa basi, nini tahadhari yake na abiria dhidi ya Uviko- 19?

Ndipo hapo mdadisi anakaa sawa kujua hulka ya kujiamini, maana mwonekano wa uzoefu wa mtumishi huyo mahali hapo, pia 'hodi' za mvi kichwani anajiamini, hakuna shaka matarajio ni kupata majibu yaliyojitosheleza.

**MAJIBU YAKE**

Mhudumu huyo anafafanua tafsiri na maoni yake, kwamba 'ugonjwa huo unawapata watu wenye fedha' na siyo walala hoi kama yeye na wanaotumia usafiri wa mwendokasi au daladala, Ni ugonjwa 'unaopenda' maeneo yenye baridi.

"Watu wanaopenda kukaa kwenye ubaridi wa viyoyozi ni wale wenye fedha. Mimi na wewe tunashinda juani kila siku, hiyo corona itatupata saa ngapi? Kesi hiyo usihofu unapoona abiria wanapanda bila kuvaa barakoa," anaeleza.

Mtendaji huyo wa mwendokasi anaendelea: "Kama hujui kuhusu corona, hiyo ndiyo elimu ninayokupa kwamba ugonjwa huu ni vigumu kuwapata walalahoi kama mimi na wewe. Ukweli ndiyo huo ili usiendelee kuhangaika!"

Ni aina ya majibu ya mtumishi wa usafiri yanayojitosheleza kutambua haja ya elimu zaidi kwa wananchi na tahadhari dhidi ya ugonjwa huo, kwani inawezekana kuwapo wengi wenye mawazo ya aina hiyo.

Msingi wake, ni kwamba kila mmoja anatakiwa kuchukua tahadhari ambazo zimekuwa zikielekezwa na wataalamu wa afya, kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa, badala ya kuzembea kwa imani wanaougua ni wenye fedha.

**VIPI MWONGOZO?**

Jambo linaloendelea sasa, ni kwamba wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania inahimiza kutopuuza ugonjwa huo, kwani iko wazi safari ya kuudhibiti inaweza kuwa ndefu.

Kuna mwongozo ulioko kwamba katika maeneo ya mikusanyiko kama vile stendi ya mabasi ya abiria na sokoni, mahitaji kama maji tiririka na barakoa ni vitu muhimu sana katika kukabili kuenea maambukizi ya Uviko - 19.

Viongozi wa mtaa au maeneo husika wanaelekezwa kuhakikisha kuna vyombo vya kuhifadhi maji na sabuni za kutosha katika kila kituo, soko au stendi, huku uongozi wa maeneo husika wakitakiwa kusimamia uwapo wa vifaa hivyo na mahitaji yake yote muhimu ikiwemo vifaa vya kunawia kwa majitiririka na kuhakikisha abiria wote wananawa.

Hapo ndipo inapoangukia haja ya vyombo vya usafiri na wakala wao kuhakikisha wanatambua nafasi ya vitakasa mikono katika vyombo vya usafiri, ili kila msafiri anayeingia katika chombo cha usafiri wa umma, lazima awe amepata huduma hiyo muhimu.

Pia, abiria wote wanatakiwa kuendelea kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutosongamana ndani ya vituo vya mabasi kupitia walinzi getini, wahudumu wa mabasi na askari wa usalama wa barabarani.

Madereva wa bodaboda nao wanaelekezwa kubeba idadi sahihi ya abiria na siyo mshikaki na wavae barakoa, huku katika stendi zikitakiwa kuhakikisha zinatoa ujumbe wa kuelimisha jamii ya wasafiri mara kwa mara.

Ujumbe wa kuelimisha jamii unaoelekezwa na mwongozo, ni ule wa kupitia vipaza sauti. Wawapo safarini, madereva na wahudumu wa vyombo vya usafiri wahakikishe elimu hiyo, inatolewa kwenye chombo kila mara.

Vyombo vya ulinzi na usalama vinapewa jukumu la kuhakikisha magari ya usafiri wa umma yanabeba abiria kulingana na idadi ya viti, pasipo kuruhusu abiria kusimama kuepusha msongomano ndani ya magari hayo.

**KULIVYO MITAANI**

Mwongozo wa Udhibiti wa Ugonjwa huo Kupitia Afya ya Kudhibiti Misongamano Katika Jamii Bila Kuathiri Shughuli za Kiuchumi, Toleo la Kwanza la Julai mwaka jana umeainisha mengi kwa kina.

Maudhui ya mwongozo huo yanatokana na kamati ya wataalamu wa afya, umeainisha maeneo mahususi yanayohitaji kutiliwa mkazo kupitia afya ya kupunguza msongamano katika jamii, ili kukata mnyororo wa maambukizi ya UVIKO-19 kuanzia ngazi ya kaya hadi jamii.

Pia, inaelekezwa kusitishwa mikusanyiko mikubwa isiyokuwa ya lazima, ikiwamo ya kijamii, kidini, kisiasa na penye ulazima wa mikusanyiko hiyo, kibali kinapaswa kuombwa.

Ufafanuzi unaanzia ofisi za serikali za mitaa, kukipatikana idhini ya halmashauri husika kutoka kofia ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa, ambazo mwenyekiti wake huwa mkuu wa mkoa husika.

Vilevile, ni mwongozo unaotaka udhibiti wa mikusanyiko katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya huduma za kijamii, kibiashara, kiuchumi, kiofisi kwa kuwa ni mojawapo ya vyanzo vya kusambaa maambukizi katika jamii.

Maeneo mengine yanayoguswa na hatari ya maambukizi ni kwenye vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, ambako ugonjwa unaweza kusambazwa zaidi, kama hakuna hatua stahiki za kuzingatiwa kukabili maradhi hayo ambukizi.

Ni mantiki inayoshuka mbali, katika maeneo ya biashara, ambako uhalisia ni mithili ya wahusika wamejiweka kando dhidi ya maradhi hayo, mikusanyiko inaendelea katika sura ya kawaida na hakuna hata viashiria vya tahadhari ya kujikinga na ugonjwa corona.

Imeelezwa rasmi kuwa hadi kufikia Desemba 18 ya mwezi uliopita watu milioni 1.27 walishapata chanjo kamili ya kujikinga na ugonjwa huo na mikoa mitano; Mwanza, Ruvuma, Mara, Kagera na Dodoma ikitajwa kuongoza utoaji chanjo na mingine; Manyara, Songwe, Njombe, Singida na Iringa inatajwa kusuasua katika harakati za chanjo.

AFYA

UKUAJI UBONGO WA MTOTO...

# Mtaalamu aanika: Fikra, mantiki, uwezo wa kutafakari umejificha katika usomaji vitabu



Mzazi akiwa na watoto akiwahamasisha kusoma vitabu. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mziray Kiraghinja, SJMC**

UPEO wa ubongo wa kibinadamu na nyenzo za kibaiolojia zinazoendana nazo, ina uhusiano wa namna ambavyo inakuzwa, suala la kujifunza lina maana kubwa katika tafsiri ya ukuaji.

Hiyo inamaanisha haja ya inayohamasishwa sasa kuanzia kliniki hadi kampeni kwenye vyombo vya habari kutoka Wizara ya Afya kuhusu ukuaji akili na afya ya ubongo .

Hapo ndipo mtoto anavyokua, pia hata kwa mtu mzima, maarifa mengi hupatikana katika usomaji vitabu na maandiko mengine kama magazeti. Hata hivyo, ni kawaida wasomaji au wenye utamaduni huo wa kusoma vitabu ni wachache, zikitajwa sababu kuu ni kama ukosefu wa vitabu, uvivu na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Hiyo ina maana gani? Pia, ukuaji akili unasuasua katika namna moja au nyingine. Usomaji unapambanua uwezo wa kuyaelewa kwa undani kinapopatikana, wazazi na walezi ndio wenye jukumu la kuwajenga watoto tangu wakiwa wadogo.

Wataalamu wana hoja kwamba utamaduni wa kusoma vitabu unakuza uwezo wao wa kufikiri na kuelimika zaidi katika masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Ndipo unapokuja uhitaji wa kuwachagulia watoto vitabu vya kusoma vinavyoendana na umri, ikiwamo michoro na rangi zinazowavutia.

Usomaji vitabu unatajwa kimantiki kusafirisha mtoto kwenda sehemu mbalimbali, anakua kiakili kwa kujengwa na matukio ya kitabuni, anatembea na mhusika katika kitabu na kujifunza vingi.

**WATAALAMU WAELEZA**

Halima Juma, Mwalimu wa Taaluma katika shule ya msingi, anaeleza elimu ni mchakato wa maarifa, tabia, mila na maadili ya jamii moja ikipitishwa kwa kizazi kimoja hadi kingine.

Anataja kuwapo aina mbili za elimu; rasmi na isiyo rasmi akifafanua isiyo rasmi inayotolewa na wakala wa maisha ya kila mtu, kwa maana ya wazazi na walezi. Usomaji vitabu kwa watoto unaingia katika aina zote za elimu.

Watoto wanajifunza maadili, mila na desturi na tabia za kijamii, ndipo msingi wa tafakari ya kujifunza vitu mbalimbali kutoka kwenye jamii inayomzunguka, ikiwamo tabia ya usomaji vitabu

Anasema mtoto wakati wote anaiga tabia ya mzazi na mlezi, pia anataja inahusu mafunzo ya kimfumo yanayotolewa na taasisi au vituo rasmi vya elimu vya umma na binafsi kwa watoto, vijana na watu wazima kwa nia ya kukuza ujuzi na maarifa.

Pia anaitaja kuwa msingi mkuu wa mtoto kujua kusoma vitabu, akianza nayo katika elimu ya awali anayokuwa nayo hadi umri wa miaka sita

Mtoto anapojifunza kusoma, kuandika na kuhesabu inawalenga watoto wenye umri wa miaka saba hadi 12, ndipo msingi mkuu wa watoto kujengewa utamaduni mzuri wa kusoma vitabu 'hunoga'.

Anaeleza ni wakati mzazi na mwalimu wanaangukia wajibu wa kuwajengea watoto mazingira mazuri ya usomaji vitabu visivyo vya mtaala.

Ofisa Mipango wa Mkataba wa asasi Realising Education for Development, Lusekelo Mwalughelo, anaeleza, mtoto anayesoma vitabu na asiyesoma vitabu wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika uwezo wa kufikiri, kuzungumza, kufanya uamuzi na kukabiliana na baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo.

Anataja sababu ni kwamba, msoma vitabu hukumbana na changamoto mbalimbali, katika harakati za kutaka kujua maarifa ambayo wanaopata wanayapitia

Pia, inamsaidia mtoto kua na utendaji mzuri katika masomo yake ya darasani na kuongeza kiwango cha kujiamini mwenyewe kupitia wahusika mbalimbali aliokuwa akiwasoma katika vitabu.

Kingine anataja wazazi hawana budi kuwa na utamaduni wa kuwanunulia vitabu watoto na hata kusoma nao walau vitabu viwili au kimoja kila wakiwa pamoja ili kukuza utamaduni huo wa kusoma.

Jarida la Science Daily la Marekani, linaeleza utafiti mpya unao onyesha kusoma vitabu na mtoto anayeanza utotoni unaweza kuongeza ujuzi wa msamiati na kusoma miaka minne, kabla ya kuanza shule ya msingi, pia inawapa watoto uwezo wa kudumu wa kusoma na kuandika.

**WAZAZI NA YAO**

Mzazi Hamis Abdul, mwenye watoto wawili, mkazi wa Mikocheni, Dar es Salaam, anaeleza sababu zinazomfanya ashindwe kuwajengea watoto wake misingi mizuri ya usomaji wa vitabu tangu wakiwa wadogo.

Anataja kuuzwa bei kubwa kunachangia ashindwe kuwanunulia watoto vitabu vya kusoma, pia vitabu vinavyoandikwa siku hizi vimekua si rafiki sana ikilinganishwa na ukuaji wa watoto.

Anasifu awali uandishi wa vitabu ulikuwa mahiri, ilhali sasa unatawaliwa na biashara lengo ni kuuza na sio kufunza zaidi, jambo ambalo hata mtaalamu Lusekelo analitaja.

Pia, anasema wao wazazi hukosa utamaduni wa kukaa na watoto kuwasomea vitabu vya hadithi kama ilivyo zama za udogo wao, ni sababu ya kupotea utamaduni wa usomaji wa vitabu kwa watoto.

Kingine kinatajwa ni maendeleo ya sayansi na teknolojia, ni miongoni mwa changamoto zinazomkumba yeye kama mzazi kushindwa kumjengea utamaduni wa kusoma vitabu mtoto wake, sasa kuna vifaa vingi vya kidigitali wakiamini ni nyenzo za kujifunza kama vitabu.

Swaumu Masoud, mwanafunzi wa shule ya msingi Gilgala darasa la nne ana ufafanuzi kwamba anashindwa kusoma vitabu kwa sababu hajawahi kununuliwa vitabu na mzazi wake, wanaoamini hawezi kuvitunza, hivyo anaishia kusoma vitabu vya kimtaala vinavyopatikana na kufundishwa shuleni.

Hassan Daud, Mwalimu wa Shule ya Msingi anayeeleza kuwa usomaji wa vitabu kwa watoto kwao umewasaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi, kwani wanajifunza misamiati mipya katika lugha na kuwa wabunifu katika nyanja mbalimbali, ikiwamo kuweka kumbukumbu ambazo hufika nazo mbali hadi kwenye masomo mengine ya mitaala.

Kwa mujibu wa Tamko la Maendeleo Endelevu ya Milenia la Mwaka 2000, Kipengele cha Pili na Tatu, vinatoa haki ya elimu kwa watoto wote na elimu ya jinsia inayolenga kukuza kujifunza.



# Bashungwa ataka vituo vya huduma kwa wateja mikoani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amemwagiza Katibu Mkuu, Prof. Riziki Shemdoe, kuweka mikakati ya uanzishwaji wa kituo cha kutolea huduma kwa mteja kila mkoa.

Bashungwa alitoa agizo hilo juzi alipotembelea kituo cha huduma kwa mteja cha Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa lengo la kuangalia maelekezo aliyoyatoa kuhusu maboresho ya kuhakikisha huduma bora inatolewa kwa wananchi.

"Nimeridhishwa na utendaji kazi wa watumishi wa kituo cha kutolea huduma kwa wateja cha Ofisi ya Rais TAMISEMI. Lakini ingekuwa vyema vituo hivyo vingekuwa vinapatikana katika ngazi ya mikoa ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma kwa haraka tofauti na sasa mpaka wapige simu wizarani kutatuliwa kero zao.

"Hivyo tuna wajibu wa kuweka mikakati ya kushusha huduma hizo mikoani kuwapunguzia adha wananchi kufuata huduma ngazi ya wizara," alisisitiza Bashungwa.

Alimwagiza katibu mkuu huyo kuhakikisha anatafuta rasilimali fedha na vifaa ili kuhakikisha mkakati wa kuweka nguvu na kuimarisha sekretarieti za mikoa katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa unafanikiwa.

Pia aliwaagiza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa ndio watakaokuwa wasimamizi wakuu wa vituo hivyo vya huduma kwa wateja lengo likiwa kuhakikisha huduma bora inapelekwa kwa wananchi kwenye maeneo yao na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma wizarani.

"Jambo hili limeanza vizuri ngazi ya wizara, hivyo tuimarishe kwenye mikoa ili kuwasaidia wananchi. Nawaagiza kuhakikisha tunaweka mikakati ya kila mkoa kuwa na kituo cha huduma kwa wateja ili wananchi wanapohitaji huduma kutoka mikoani wanakuwa na namba ambazo wanaweza kupiga badala ya kutoka vijijini kuja kupata huduma wizarani," alisisitiza.

Msimamizi wa kituo cha huduma kwa wateja, Antelma Mtemahanji, alisema lengo la kuanzishwa kwa kituo hicho ni kuwasaidia wananchi waliokuwa wakitembea umbali mrefu kutoka vijijini kufuata huduma mbalimbali za kiofisi.

Alisema toka kituo kimeanzishwa mwaka 2020 hadi sasa, simu 125,381 zilizopokewa na kufanyiwa kazi.

Kwa mujibu wa Mtemahanji, kabla ya kuanzishwa kwa kituo hicho, TAMISEMI ilikuwa ikipokea wateja 100 hadi 120 ambao walikuwa wakifika ofisini kufuata huduma. Lakini hali hiyo kwa sasa imepungua na kuondoa mrundikano wa wananchi kufuata huduma wizarani.



Mratibu Mkuu wa mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma shirikishi za afya kwa watu wenye ulemavu, Askofu wa Kanisa maalum la watu wenye ulemavu wa kusikia (Viziwi) la Betheli Baptisti Tanzania (KVBBT), Frank Sarungi, akitoa mafunzo kwa wataalamu wa afya na ustawi wa jamii wa Jiji la Dodoma jana, kuhusu jinsi ya uelewa wa kuwahudumia watu wasiosikia. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Hospitali mikoa zapewa kibarua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HOSPITALI za rufani za mikoa nchini zimetakiwa kuboresha huduma za afya pamoja na kuwa na mawazo mapana katika uboreshaji wa miundombinu ili kuisaidia kuipunguzia mzigo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa idara ya tiba ikiwa ni mwendelezo wa kukutana na kufanya mapitio ya idara mbalimbali zilizoko kwenye wizara hiyo.

Ummy alisema ili kuonyesha kweli idara ya tiba ndio inayobeba wizara hiyo hamna budi kuboresha huduma hizo ili zilingane na mahitaji ya wananchi kwani wananchi wanaziamini hospitali za umma.

"Tunatakiwa kuhakikisha utoaji wa huduma za afya ni mzuri, hivyo ni wakati wa kuangalia changamoto na kuziboresha ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi ambao wanafika kwenye vituo vyetu kupata huduma," alisema.

Waziri Ummy aliitaka idara hiyo kufanya upya mapitio ya miongozo ya utoaji huduma ili kufanya huduma zinazotolewa kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa zinakuwa bora na zenye manufaa kwa wananchi.

Vilevile alisema miongozo hiyo iweze kuunganisha vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Ummy aliwataka watumishi wa idara hiyo kufanya kazi kama timu na endapo kuna changamoto ni vyema zikajadiliwa kwa pamoja ili kwenda kwa pamoja katika kuboresha huduma za afya nchini.

# Watoto wa mitaani wapaza sauti kwa waziri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATOTO waishio katika mazingira magumu kwenye Jiji la Dodoma wamemweleza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, madhila wanayokumbana nayo huku wakiomba serikali kuwanusuru kwa kuwa si kusudi lao kuishi hivyo.

Hayo yalijiri juzi wakati waziri alipoongoza jopo la wataalamu wa wizara hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenda mitaani wanakoishi watoto hao kwa ajili ya kuzungumza nao na kujifunza serikali inawezaje kuwabadilishia maisha yao yawe na ustawi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watoto hao waliofikiwa na jopo hilo walisimulia madhila na matatizo wanayopitia wakiwa katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

"Sisi watoto tuishio katika mazingira ya mitaani tunapitia madhila mengi sana, tunalazimika kutumia vilevi, kujifunza mambo mengi mabaya pia tunafanyiwa mambo mabaya na tunalazimika kuwa watu wasio wema ili tuishi. Matokeo yake tunabaguliwa na kutengwa na jamii," alisema mmoja wa watoto (jina limehifadhiwa).

Mtoto huyo pia alisema wako baadhi yao wamekuwa wakipitia ukatili wa kupigwa na wenzao wanaowazidi umri, wanaofanyiwa ukatili wa kingono na kuambukizwa magonjwa.

Dk. Gwajima, akizungumza na watoto hao aliwaeleza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuboresha ustawi wa watoto na ameunda wizara mpya ambayo pamoja na mambo mengine, itasimamia maendeleo na ustawi wa makundi maalumu ikiwamo watoto kwa ujumla wake.

"Hivyo ziara hii ya kujifunza huu ni mwanzo wa safari ya kuwaondoa watoto wanaoishi mitaani wakaishi maisha salama na yenye ustawi, hivyo wananchi na watendaji toeni ushirikiano kwani ufumbuzi wa jambo hili utatokana na wanajamii wenyewe," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema tayari ameanza kuratibu ushirikiano na makatibu wakuu wa wizara zingine katika operesheni hiyo kubwa ya kuwarejesha watoto wa mitaani kwenye maisha yenye ustawi na atasimamia jambo hilo kwa ushirikiano na wadau wengine wote.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kaspar Muya, alisema ofisi hiyo iko tayari kuratibu ushirikishwaji wa wizara na sekta zote, ili jambo hilo lifanikiwe kama ilivyokusudiwa kwenye Mpango wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA, 2017/18-2021/22) na Ilani ya Uchaguzi Mkuu CCM ya mwaka 2020-2025.

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu imeanza kuratibu kuwezesha watoto waishio kwenye mazingira hatarishi kurejea kwenye maisha yenye ustawi ili wakiwa watu wazima wachangie maendeleo ya taifa kwa tija.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, alisema mkoa uko tayari kushirikiana na wadau wote kusimamia utekelezaji wa jambo hilo kwa ufanisi.

Ziara hiyo imefanikisha kuwarejesha watoto 14 kwenye makao ya watoto na uratibu unaendelea mkoani Dodoma na utaendelea katika mikoa yote nchini.





# Asilimia 90 waripoti kidato cha kwanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya asilimia 90 ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule mbalimbali mkoani Mbeya wameshariipoti shuleni ikiwa ni siku tatu baada ya shule za msingi na sekondari kufunguliwa.

Aidha, wanafunzi wa darasa la kwanza na darasa la awali walioripoti wamefikia zaidi ya asilimia 100, hali ambayo inadaiwa kusababishwa na serikali kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya shule hasa vyumba vya madarasa.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera kwenye ukaguzi wa mahudhurio.

Dk. Chuachua alitembelea baadhi ya shule za msingi na sekondari jijini Mbeya kukagua mahudhurio ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, darasa la kwanza na darasa la awali huku akiwa ameambatana na baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama.

Mwalimu Hinju alisema wanafanya mawasiliano ya kiofisi na halmashauri zote za mkoa wa Mbeya kubaini hali ya mahudhurio ili kujua kama kuna sehemu ina tatizo lolote ili litatuliwe mapema na wanafunzi waendelee na masomo bila kikwazo.

Alisema kwa taarifa za awali mahudhurio katika halmashauri zote za mkoa huo wanafunzi wameitikia vizuri na hata wazazi wamejitolea vizuri kuhakikisha watoto wao wanaingia shuleni.

"Pamoja na mahudhurio haya ambayo mnayaona, lakini bado wanafunzi wanaendelea kujitokeza na mawasiliano yetu yanaonyesha kila wilaya hali iko hivi hivi, kwa hiyo nikuhakikishie Mkuu wa Wilaya kwamba zoezi linaenda vizuri," alisema Mwalimu Hinju. Baadhi ya walimu wakuu na wakuu wa shule walisema mwitikio huo wa wanafunzi unachangiwa na vitu vingi ikiwamo ushirikiano kati ya uongozi wa serikali za mitaa, wazazi na shule zenyewe.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Iganzo jijini hapo, Cliff Gasper, alisema wazazi wengi wameitikia kuwapeleka watoto wao shuleni kutokana na kutokuwapo kwa michango ya aina yoyote shuleni zaidi ya kununua sare na vifaa vingine kwa ajili ya watoto wao.

Alisema awali wazazi wengi walikuwa hawana mwitikio wa kuwapeleka watoto wao shuleni kutokana na kuepuka michango iliyokuwa inatozwa ikiwamo ada, lakini kwa sasa kikwazo hicho kilishaondolewa na serikali kwa kufuta michango.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Chuachua alisema kwa mara ya kwanza mwaka huu wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza pamoja tofauti na miaka mingine ambayo wengine walikuwa wanachelewa.

Alisema miaka ya nyuma baadhi ya wanafunzi walikuwa wanachelewa kwa sababu ya kukosa miundombinu hasa vyumba vya madarasa na madawati, lakini kwa mwaka huu kikwazo hicho hakipo.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza (kushoto), akizungumza kuhusu umuhimu wa barabara ya Izumbwe - Igale – Iyunga, wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ya kukagua miradi ya maendeleo hivi karibuni. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bei ya mbolea yaendelea kuibua kilio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Wilaya ya Mbeya, wameendelea kulalamikia bei ya mbolea ambapo wamesema kuna hatari mwaka huu mavuno ya mazao ya chakula hasa mahindi ukashuka kutokana na wengi wao kushindwa kumudu bei ya mbolea.

Pia wamesema hali hiyo inaweza kusababisha njaa. Waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Jimbo hilo, Oran Njeza ambaye alikuwa anasikiliza kero za wananchi katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo, ambapo walisema wana wasiwasi kutokana na wakulima wengi kushindwa kumudu bei.

Jailos Mwakanyamale Mkazi wa Kata ya Iwindi, alisema kwa sasa mahindi yamefikia hatua ya kukuzia lakini mpaka sasa wanashindwa kukuzia kutokana na bei ya mbolea kuwa juu.

Alisema mbolea ya kukuzia ambayo walikuwa wananunua Sh. 40,000 mpaka 50,000, lakini kwa sasa inauzwa Sh. 105,000 na kwamba ili mtu akuzie ekari moja anatakiwa kuwa na mifuko miwili.

Alisema kwa sasa bidhaa hiyo inapatikana kwa wingi madukani, lakini tatizo lililoko ni bei kubwa ambayo inawashinda wakulima wengi hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema endapo uzalishaji utapungua kuna hatari pia ya uchumi wa wananchi ukashuka kwa maelezo kuwa uchumi wao unategemea zaidi kilimo.

"Hili tatizo la mbolea sasa hivi limekuwa kubwa mno, kilimo sasa hivi kitakuwa cha matajiri pekee, sisi wengine tutakuwa tunalima mazao kwa ajili ya kututosheleza sisi na familia zetu, huwezi ukalima kwa ajili ya kuuza," alisema Mwakanyamale.

Naye Sajila Kilembe aliiomba serikali iwe na utaratibu wa kudhibiti bei ya pembejeo zote ili kuimarisha sekta ya kilimo ambayo ni miongoni mwa sekta zinazoliingizia taifa fedha nyingi pamoja na kulihakikishia taifa usalama wa chakula.

Alimwomba mbunge wa jimbo hilo, Njeza kuwasaidia kuwasilisha kilio chao serikalini ili wasaidiwe na kwamba ikiwezekana serikali iwaingizie ruzuku kwenye pembejeo ili bei zipunguwe.

Akijibu malalamiko ya wananchi hao, Njeza alisema ili kuwasaidia wakulima ameshaanza mazungumzo na baadhi ya wadau wanaosambaza pembejeo ili wawasaidie kupunguza bei ya mbolea.

Alisema serikali pia inaendelea na michakato mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la mfumuko wa bei ya mbolea ikiwamo kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea kwa wingi kutoka nje na kuwashawishi wapunguze bei.

"Ni kweli kwa sasa bei ya mbolea iko juu na hii imesababishwa na tatizo la corona, wamiliki wengi wa viwanda wamepunguza uzalishaji na baadhi wamefunga viwanda, sasa kwa kawaida kitu kikipungua ni lazima bei yake ipande," alisema Njeza.

Hata hivyo, alisema kwa sasa madhara ya corona yameanza kupungua na hivyo uzalishaji wa mbolea na bidhaa zingine duniani utaongezeka na hivyo kuna matumaini ya bei kupungua.

Vilevile, alisema serikali imeanza mikakati ya kufufua viwanda vya kuzalisha mbolea ili kupunguza utegemezi wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Aliwataka wakulima kuendelea kuzalisha mazao kulingana na uwezo wao ili wasije wakakosa chakula kwa kisingizio cha kukosa mbolea huku akiwataka kutumia pia mbolea za asili.

# Waomba maboresho barabara za mitaani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Gombe Kusini Kata ya Itezi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kuwaboreshea barabara za mitaa wakidai kuwa mvua ikinyesha maji yanakosa uelekeo na kujaa kwenye nyumba zao.

Wakizungumza na Nipashe jana wananchi hao walisema barabara za mitaani zipo, lakini hazijawekewa miundombinu mizuri ya maji, hali ambayo inasababisha mafuriko kwenye maeneo ya makazi yao.

Hamis Mwasenga aliiomba serikali kuwaboreshea miundombinu hiyo kutokana na kuwa tatizo hasa kipindi hiki cha mvua nyingi kunyesha, akidai kuwa kutokana na makazi holela maji hayana uelekeo.

Alisema wakati mwingine huwa wanalazimika kuwapeleka watoto wao shuleni na kwenda kuwachukua wakati wa kurudi kutokana na kuhofia kusombwa na mafuriko.

"Kama unavyoona hapa maji huwa yanajaa na hayana kwa kwenda, hizi nyumba maji huwa yanaingia miaka yote kutokana na maji yanayotoka kule juu yanakuja kupita hapahapa," alisema Mwasenga.

Naye Neema Mwaijande alisema barabara ya lami imepita upande wa Gombe Kaskazini, lakini mifereji mingi imeelekezwa upande wao hali ambayo pia imechochea mafuriko kwenye maeneo yao.

Alisema katika eneo hilo kuna watu wengi ambao wanategemea barabara hiyo inayounganisha mtaa wao na Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM).



# TAMWA yashtuka ongezeko la matukio ya ukatili, udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema licha ya adhabu kubwa inayotolewa kwa washtakiwa wa kesi za udhalilishaji, anashangaa kuwa matukio ya udhalilishaji yanaongezeka Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa masuala ya udhalilishaji uliolenga kujadili changamoto, mafanikio na nini kifanyike kutokomeza vitendo vya udhalilishaji.

Hata hivyo, Dk. Mzuri alisema hukumu za kesi za udhalilishaji zinazotolewa na mahakama zinaridhisha ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Mkurugenzi huyo alisema anashangaa kuona matukio ya udhalilishaji yanaongezeka licha ya kwamba adhabu kubwa zinatolewa kwa washtakiwa wa makosa hayo.

"Hukumu zinazotolewa kwa washtakiwa wa kesi za udhalilishaji zinaridhisha. Tunashuhudia hukumu zinatolewa miaka 30 hadi 80, lakini sijui kwa nini matukio yanaongezeka," alisema Dk. Mzuri.

Kwa mujibu wa Dk. Mzuri, matukio ya udhalilishaji, yakiwamo ya ubakaji, yamekuwa yakifanywa na watu wa karibu katika familia wakiwamo kinababa kubaka watoto wao.

Dk. Mzuri alisema lazima kuwe na mikakati mipya ya ulinzi mkubwa kwa wanawake na watoto ili kutofanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Hamad Kombo, alisema mashahidi bado ni kikwazo katika kutoa ushahidi mahakamani hasa kwa waathirika wenyewe wa kike wenye umri kati ya miaka 14 hadi 17 ambao wamefanyiwa vitendo vya ubakaji.

Alisema waathirika hao wa udhalilishaji huwa wanawalinda wadhalilishaji kwa kutoa ushahidi wa uongo mahakamani au kukataa kutoa ushahidi kwa sababu huwa ni wapenzi.

Naye Ispekta wa Polisi kutoka dawati la jinsia Mkoa wa Kaskazini Pemba, Fakihi Yussuf, alisema wanafanya kazi katika mazingira magumu kufanya upelelezi wa kesi za udhalilishaji.

"Mimi binafsi natoa fedha zangu mfukoni kuwafuata mashahidi wa kesi za udhalilishaji wakati ninapofanya upelelezi wa kesi hizi. Polisi tunafanya kazi katika mazingira magumu katika mapambano ya kesi za udhalilishaji," alisema.

Kuhusu mafanikio katika mapambano ya kesi hizo, alisema kesi zinafikishwa mahakamani kwa haraka na kesi 15 zimetolewa hukumu kwa mwaka jana kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kesi 168 za udhalilishaji zimeripotiwa polisi katika mkoa wa Kaskazini Pemba na kesi 144 zimeripotiwa mkoa wa Kusini Unguja ambapo asilimia 20 ya watuhumiwa wa kesi hizo wamekimbia na bado hawajapatikana.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (kushoto), akizungumza katika mkutano wa kujadili sheria ya habari Zanzibar, uliofanyika Tunguu, kisiwani hapo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ufaulu mitihani kidato cha nne 2021 wapanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imetoa taarifa ya tathmini ya matokeo ya kidato cha nne mwaka 2021 inayoonyesha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar kimeongezeka kulinganisha na matokeo ya mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari wa Wizara hiyo, Asya Iddi Issa, alisema watahiniwa 24,051 waliandikishwa na 23,557 sawa na asilimia 97.95 walifanya mtihani huo. Alisema watahiniwa 494 sawa na asilimia 2.05, hawakufanya mtihani kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo maradhi, vifo na utoro.

Alisema kwa upande wa Zanzibar watahiniwa 15,569 sawa na asilimia 66.09 wamefaulu na kusababisha ufaulu kuongezeka kwa asilimia 8.59 kulinganisha na mwaka 2020 ambao ulikuwa asilimia 57.5

Mkurugenzi huyo alisema bado jitihada za makusudi zinahitajika ili kuhakikisha ufaulu kwa daraja la kwanza unaongezeka zaidi.

Alisema ili kuondosha kabisa alama ya zero, ushirikiano unahitajika baina ya walimu, wazazi, wanafunzi na jamii nzima.

Matokeo hayo ya kidato cha nne kwa mwaka 2021 kwa Shule za Zanzibar, alisema yanaridhisha kutokana na kupungua kwa alama za zero na kuongezeka kwa ufaulu wa daraja la kwanza.

Alisema wanafunzi waliopata ufaulu wa daraja la kwanza kwa Zanzibar ni 445 sawa na asilimia 1.89, daraja la pili ni 1,302 sawa na asilimia 5.53 na daraja la tatu ni 2,621 sawa na asilimia 11.13.

Kwa waliopata daraja la nne, alisema ni 11,201 sawa na asilimia 47.55 na waliopata alama zero ni 8,111 ambao ni asilimia 34.43.

**Alisema ili kuondosha kabisa alama ya zero, ushirikiano unahitajika baina ya walimu, wazazi, wanafunzi na jamii nzima.**

# Waziri Saada Mkuya ataka habari zenye takwimu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amewataka waandishi wa habari kuandika habari za takwimu ambazo zina uzito mkubwa ikilinganishwa na zile zinazoandikwa bila ya takwimu.

Dk. Mkuya alisema hayo jana katika hafla ya sherehe za tuzo za uandishi wa habari za takwimu kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake ambazo zimeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Alisema waandishi wa habari wanapoandika habari za takwimu zenye uwiano wa wanawake na wanaume katika uongozi na nyanja za kiuchumi, watasaidia kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi hizo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, ili kuwe na usawa wa kijinsia, vyombo vya habari vinapaswa kuweka uwiano sawa kati ya habari za wanawake na wanaume.

Waziri Mkuya aliipongeza TAMWA kwa juhudi inazozichukua katika kujenga uwelewa kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia.

"Pia niwapongeze waandishi wa habari waliothubutu kuwasilisha kazi zao katika mashindano haya na wale ambao hawakushinda kutovunjika moyo na badala yake kuongeza juhudi ili kuwa na kazi bora," alisema.

Akitoa taarifa ya mashindano hayo, mwenyekiti wa jopo la majaji wa tuzo hiyo, Imane Duwe, alisema kazi 452 kutoka redio, magazeti, runinga na mitandao ya kijamii ziliwasilishwa.

Duwe alisema ili kupata washindi, vigezo vilitumika ikiwamo upekee wa mada, mtiririko wa uwasilishaji, matumizi ya takwimu, uwiano wa vyanzo kati ya wanawake na wanaume.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema tuzo hizo zimebuniwa ili kuongeza umahiri katika uandishi wa habari za uongozi kwa wanawake.

Katika tuzo hizo, mshindi wa kwanza kwa upande wa magazeti aliibuka Husna Muhamed wa gazeti la Zanzibar Leo na mwandishi wa Nipashe, Rahma Suleiman, aliibuka mshindi wa tatu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA UKAGUZI, WA ELIMU SIFA AWE NI MKAGUZI WA ELIMU MSTAAFU**
**0783 298 900**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAMIS NSOLEZI LWIBIKILE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2699/0080** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya WEMA mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIL/RB/22995/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ALIKO AMBOKILE MWASAMWAJA,** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T.135 AEJ.** Yeyote atakayeiona atowe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi **MBE/TUK/RB/23261/2020**

## TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED

**TANGAZO LA MNADA NA NOTISI**

**Kesi No. 51/2021** mdai Joyce Gidion Lufumba. Mdaiwa: Nakuvanda Chilipweli

Kwa Mamlaka tuliyopewa na Mahakama ya Mwanzo Kimara tutakuwa na Mnada wa hadhara.

| MALI INAYOUZWA | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| Nyumba nzuri ya kisasa na uwanja wake | Kimara kwa Msuguri, mtaa wa mji mpya | 24/1/2022 muda ni saa nne asubuhi. |

**TARATIBU ZA MNADA**

1. Siku ya mnada italipwa 25% baada ya mnada 75% ndani ya siku 14.
2. Mali inauzwa na eneo lake kama lilivyo.

**Watu wote mnakaribishwa.**
**Simu namba 0719 187 677.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya Morogoro Kituo cha Mjini**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na...144...2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: CANDIDUS NGALEKA NDUNGURU WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: DOMINICA GRACEANN NGALEKA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24/01/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 23/12/2021** ..................
HAKIMU

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUFUNGA KAMPUNI

Tunapenda kuutangazia umma kwamba uongozi wa kampuni ya **MAKIGU INVESTMENT COMPANY LIMITED** yenye usajili namba **120842** wameamua kufunga kampuni hiyo kuanzia tarehe **09/10/2021** ambapo mkutano mkuu ulikaa na kukubaliana .

Kwa mawasiliano au taarifa
**WASILIANA 0755406076 AU 0712 889045**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# ZFF YAJIPANGA KUREJESHA MICHUANO YA MUUNGANO

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesema linajipanga kufanya kikao na wenzao wa Bara (TFF), kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kurejesha mashindano ya Kombe la Muungano ili kuzisaidia timu zao zinazoshiriki michuano ya kimataifa, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe, Rais wa ZFF, Abdul-latif Ali Yassin, alisema anaamini kufanyika kwa mashindano hayo kutaboresha na kuziimarisha timu za visiwani humo kwa ajili ya kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wanayoshiriki kila mwaka.

"Mipango yangu ni kuhakikisha ninakutana na viongozi wa Bara (TFF), kwa ajili ya kurejesha michuano hiyo hasa kuzipa nafasi timu zinazokwenda kucheza Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Yasin.

Aliongeza pande hizo mbili zitakapofikia makubaliano, watashirikisha pia serikali zote ili kutafuta fedha zitakazosaidia kuandaa michuano hiyo.

"Miaka ya nyuma Kombe la Muungano lilikuwa na timu kutoka Bara na Visiwani kwa ajili ya kupata mwakilishi mmoja, kwa sasa iwe tofauti kwa sababu kila sehemu zinatoa timu, na kwa bahati Bara wao wamepata bahati ya kuwakilishwa na timu nne."

"Tukipata nafasi ya kuanzisha kombe hilo na kupata wadhamini ambao watatupatia kiasi cha fedha mfano wakatenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya zawadi kwa timu zote, yatafanyika na malengo yatafikiwa," alisema rais huyo wa ZFF.

Kiongozi huyo alisema pia sehemu ya fedha za udhamini zitakazopatikana zitatendwa ili kuzisaidia timu hizo katika maandalizi ya safari watakapokwenda kucheza michezo ya ugenini.

"Nina imani kombe hilo halitasaidia kwa visiwani pekee kwa kurejesha ubora wa soka lakini litawezesha timu za Bara kupata fedha na kusaidia gharama za safari za kwenda kucheza mechi za ugenini," Yasin aliongeza.

Alisema alisikitishwa na kitendo cha timu mojawapo hapa nchini (hakutaja jina), ilishindwa kwenda ugenini kucheza kwa sababu ya kukosa nauli jambo ambalo liliwaumiza wadau wa kandanda na haipaswi kujirudia.

"Msimu uliopita kuna timu ilishindwa kusafiri kwenda katika mchezo wa marudiano kutokana na ukosefu wa fedha, nina imani tukianzisha Kombe la Muungano kwa njia hii itasaidia timu kufanya vizuri lakini, pia itawabeba kiuchumi," aliongeza Yasin.

Kwa sasa mashindano pekee ambayo yanazikutanisha timu za Bara na Visiwani ni michuano ya Kombe la Mapinduzi inayofanyika Zanzibar kila mwaka na wenyeji wameshindwa kung'ara kwa muda mrefu.



Wafanyakazi wa Yanga ya jijini Dar es Salaam wakiandikisha wanachama wapya na wazamani wa klabu hiyo kwa njia ya mtandao katika mchakato unaoendelea kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Nyota Tanzanite kurejea kesho

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI nyota wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), Enekia Kasonga anatarajiwa kutua nchini kesho, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema nyota wake wanaendelea vyema na maandalizi.

Enekia anacheza soka la kulipwa nchini Morocco sambamba na Mwanahamisi Omary na Diana Lucas wanaoichezea Twiga Stars.

Tanzanite Queens inatarajia kuikaribisha Ethiopia katika mechi ya raundi ya nne ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia U-20 itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Shime aliliambia gazeti hili programu za mazoezi za timu hiyo zinaendelea vizuri na anafurahishwa na ushindani unaoonekana kwenye kikosi chake tangu walivyofika Zanzibar.

Kocha huyo alisema anahitaji kupata mechi nyingine ya kirafiki ili kuwaimarisha wachezaji wake na maandalizi yameshafanyika ili kujipima dhidi ya Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya Wavulana ya umri chini ya miaka 16 ya Zanzibar

"Tumecheza mchezo mmoja dhidi ya Kombaini ya Zanzibar, tumeona kikosi kipo vizuri na nimeona maeneo gani ambayo ninapaswa niyafanyie kazi kabla ya mechi dhidi ya Ethiopia, lakini kwa asilimia zote tumejiandaa kushinda," alisema Shime.

Kocha huyo amewaomba mashabiki wa soka Zanzibar kujitokeza kwa wingi kuishangilia Tanzanite Queens kwa sababu ni timu yao na inapeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo.

# Usajili Zanzibar mwisho Jan. 31

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeongeza muda wa kukamilisha usajili na uhamisho wa dirisha dogo hadi kufikia Januari 31, mwaka huu.

Awali dirisha dogo la usajili wa wachezaji lilitarajiwa kufungwa leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Hashim Salum, alisema sababu kuu iliyopelekea kuongeza muda wa usajili ni kutokana na maombi yaliyowasilishwa na timu mbalimbali pamoja na wanachama wa ZFF ngazi ya mikoa.

Salum alisema baada ya bodi ya ligi kuridhia, wanazikumbusha timu zote kutumia vyema muda wa nyongeza uliotolewa na kuwakumbusha hakutakuwa na uamuzi mwingine baada ya dirisha kufungwa.

Hata hivyo kiongozi huyo alisema kwa ujumla zoezi la uhamisho na usajili wa wachezaji linaendelea vizuri na baadhi ya timu zimeshakamilisha mchakato huo kwa wakati.

"Tunawapongeza wale ambao wameshakamilisha mchakato huu na tayari wameanza kuwatumia wachezaji wao wapya katika michuano ya Kombe la FA inayoendelea," alisema kiongozi huyo.

# Tigers Queens yaipania Mlandizi

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa The Tigers Queens, Ezekiel Chobanka, amesema kikosi chake kiko imara na kimejiandaa kwenda kuchukua pointi tatu katika mechi yao ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Mlandizi Queens itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Mlandizi, Mabatini mkoani Pwani.

Chobanka aliliambia gazeti hili ameyafanyia kazi mapungufu waliyoyabaini katika kikosi chao ikiwamo kuimarisha safu ya ulinzi na ushambuliaji kwa ajili ya kupata matokeo mazuri.

Kocha huyo alisema pia wamewaangalia wapinzani wao na kufahamu ubora wao ili kujipanga kuwazuia na hatimaye kuondoka na ushindi wa ugenini.

"Ligi ya msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imejipanga vizuri, lakini hatujali hilo tunapambana kuboresha kikosi chetu ili kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi iwe ugenini au nyumbani," alisema Chobanka.

Alisema wanahitaji kupata pointi tatu muhimu ili wapande katika msimamo wa ligi hiyo na hatimaye kutimiza malengo ya kuwania ubingwa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### POGBA, KESSIE WANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, 28, na kiungo wa kimataifa wa Ivory Coast, Franck Kessie (25), kutoka Manchester United na AC Milan. Hatua hiyo pia inatarajiwa kumshawishi mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (23), kubakia katika klabu hiyo licha ya kuwa ananyatiwa na Real Madrid. ***(ESPN)***

#### MOURINHO: SIONDOKI ROMA

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, 58, amesema amejitolea kwa klabu hiyo na kujitenga na Everton baada ya madai kuibuka kuwa ni mmoja wa makocha wanaopigiwa upatu kuchukua nafasi ya Rafael Benitez. ***(Sky Sports)***

#### ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanafikiria kumsajili mshambuliaji wa timu ya Adana Demirspor na Italia, Mario Balotelli, 31, kwa mujibu wa rais wa klabu hiyo ya Uturuki, Murat Sancak. ***(Inside Futbol via Star)***

#### JUVENTUS, MARTIAL WATETA

JUVENTUS wamefanya mazungumzo na mshambuliaji wa Ufaransa na Manchester United, Anthony Martial, 26, lakini mabingwa hao wa Serie A bado hawajawasiliana na klabu hiyo ya Old Trafford kuhusu uhamisho wa mchezaji huyo. ***(Goal)***

#### MELO ATAKIWA ARSENAL

JUHUDI za Arsenal za kumsajili kiungo wa kati wa Brazil na Juventus, Arthur Melo, 25, zimeimarika baada ya klabu yake ya Itaila kuanza mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Lyon, Bruno Guimaraes, 24, kuchukua nafasi hiyo. ***(Get French Football via Sun)***

#### ZAKARIA KUMRITHI MELO

JUVENTUS pia wamewasiliana na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uswisi na Borussia Monchengladbach, Denis Zakaria mwenye umri wa miak 25 ili kuchukua nafasi ya Arthur Melo. ***(90min)***

#### VLAHOVIC AIKATAA ARSENAL

ARSENAL wamepata pigo katika juhudi zao za kumsaka mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic, 21, baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia kudai anataka kujiunga na Juventus. ***(Mail)***

#### SPURS YAMKOMALIA TRAORE

KLABU ya Tottenham Hotspur bado wanajaribu kumsajili winga wa Hispania, Adama Traore, 25, Januari hii licha ya kocha wa Wolves, Bruno Lage kumtaka kiungo huyo kubakia katika klabu hiyo hadi mwisho wa msimu. ***(Fabrizio Romano)***

#### NDOMBELE, ALLI KUUZWA

TOTTENHAM Hotspur inajaribu kuwauza wachezaji wake, Tanguy Ndombele, 25, beki Matt Doherty (30), kiungo wa England, Dele Alli (25) na winga wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Steven Bergwijn (24). ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: WACHEZAJI CHELSEA WAMECHOKA

**Kocha huyo asema sababu kubwa ni kikosi chake kukabiliwa na mechi...**

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amesema wachezaji wa Chelsea “wamechoka kiakili na kimwili” baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Brighton na kuwaacha wakishinda mchezo mmoja tu kati ya saba katika Ligi Kuu England.

**Kwa sasa Chelsea imepitwa pointi 12 na vinara Manchester City.**

Blues hao walianza kwa kuongoza katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amex kwa bao la pili, Hakim Ziyech, lakini walishindwa kulilinda, waliruhusu kufungwa kipindi cha pili kwa kichwa cha Adam Webster kutokana na kona.

Sasa wamechukua pointi tatu kutoka zile zilizotakiwa 12 kwa kipindi cha siku 21 na kuwafanya wakicheza mechi saba katika mashindano yote.

Huku wakiendelea kupambana kwenye mashindano mengine - ikiwamo Kombe la Carabao ambapo wamefuzu fainali wiki iliyopita - wanaonekana katika mbio za kuwania kuwafukuzia Manchester City zinaanza kufifia.

“Tunaonekana tumechoka kwa sababu tunacheza dhidi ya timu imara, tulijiandaa vizuri dhidi ya Brighton,” alisema Tuchel akiiambia BBC Radio 5 Live.

“Kama ukiangalia ratiba yetu, angalia tulikotoka, tumekuwa na wakati mgumu. Unapokuwa umechoka kiakili na kimwili - unakuwa hauko kwenye nafasi nzuri ya kujikita kwenye mechi zako. Unaweza kuona katika mechi zetu, lakini tunajua wapi tunatoka. “Naweza pia kujihisi mwenyewe. Kuna wakati unaingia kwenye basi na kukaa kwenye kiti na kufikiria tunakwenda wapi?’

“Unatakiwa kujikita na kufikiria wapi tunakwenda, lini tutakuwa pale, muda gani tutacheza na lini tutacheza tena?

LIVE IN PLAY | CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 861,

MECHI KALI
ATHLETIC BILBAO
VERSUS
BARCELONA
1 | 3.16
X | 3.21
2 | 2.24

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JUVE YAKATAA KUMSAJILI MARTIAL




**TURIN,** Italia

JUVENTUS imeondoa uwezekano wa kumsajili nyota wa Manchester United, Anthony Martial baada ya kuona ni gharama kubwa kumleta nyota huyo raia wa Ufaransa.

Ofisa Mtedaji Mkuu wa Juventus, Maurizio Arrivabene, amesema gharama zilizotajwa kwa ajili ya kumsajili fowadi huyo ni kubwa zaidi.

Martial hakuwapo katika kikosi cha Manchester United kilichomaliza kwa sare ya mabao 2-2 Jumamosi kwenye Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa, ambapo kocha wa muda, Ralf Rangnick alieleza inatokana na mchezaji mwenyewe kutokuwa tayari kujumuishwa.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alikataa madai hayo na wawili hao walionekana kuingia kwenye malumbano.

Mchezaji huyo wa zamani wa Monaco, Martial amefunga mabao 79 tangu alipoanza kuichezea United Septemba 2015 - ni Marcus Rashford pekee aliyefunga mabao mengi (91) kwa klabu hiyo kwa kipindi hicho.

Lakini alicheza dakika 358 katika kipindi cha kwanza cha msimu huu, akifunga mara moja, na kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuondoka Januari hii ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2024.

Juventus imekuwa ikihusishwa na usajili wa mchezaji huyo, lakini Arrivabene ameiambia Sport Mediaset: "Kwa uhakika kabisa sio kwa kiwango hicho cha gharama. Hatusubiri wao kushusha bei, hatutasubiri kabisa. Hatuzungumzii kuhusu hilo."



## Madrid yakubali kumuuza Hazard

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kukubali dau la pauni milioni 50 kutoka kwa Newcastle United kwa ajili ya kumuuza, Eden Hazard, lakini taarifa zinasema winga huyo amekataa kuhamia St James' Park.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameku- wa akihusishwa na tetesi za kuondoka Santiago Bernabeu, kutokana na kuwa kwenye kiwango kibaya huko Hispania, ambayo imefanya kiwango chake kuteremka hadi kupitwa na Vinicius Junior, Rodrygo na Marco Asensio.

Los Blancos wanaamini- ka kuwa tayari kuruhusu wachezaji sita wa kikosi cha kwanza kuondoka klabuni hapo Januari na Erling Hazard ni mmo wa wachezaji ambao wa tayari kujadiliana kuhu ofa zao.

Kwa mujibu wa El N cional, Newcastle Unit wamewasilisha ombi awali la euro milioni 10 kuongeza nyongeza, a bayo imekubaliwa na r wa Real Madrid, Flore tino Perez.

**HABARI MICHEZO**


# 636,800

## JACKPOT MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/01/22 | 18:00 | Zaragoza vs Valladolid | 2.94 | 3.08 | 2.41 |
| 02. 22/01/22 | 18:30 | Moreirense vs Santa Clara | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 03. 22/01/22 | 20:15 | Fuenlabrada vs Las Palmas UD | 2.99 | 3.04 | 2.40 |
| 04. 22/01/22 | 21:00 | Tondela vs FC Vizela | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 05. 22/01/22 | 23:00 | Malaga vs UD Ibiza Eivissa | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/01/22 | 16:00 | Granada vs Osasuna | 2.51 | 3.16 | 2.91 |
| 07. 23/01/22 | 16:00 | Burgos vs Leganes | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 08. 23/01/22 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.63 | 3.18 | 2.63 |
| 09. 23/01/22 | 19:00 | Galatasaray vs Trabzonspor | 2.55 | 3.19 | 2.70 |
| 10. 23/01/22 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.80 | 2.95 | 2.75 |
| 11. 23/01/22 | 22:00 | Waalwick vs Fortuna Sittard | 2.32 | 3.35 | 2.85 |
| 12. 23/01/22 | 22:45 | AC Milan vs Juventus | 2.66 | 3.26 | 2.66 |
| 13. 23/01/22 | 23:00 | Alcorcon vs Mirandes | 2.65 | 3.09 | 2.65 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 20/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4964 | Galatasaray U19 vs Kasimpasa U19 | 1.27 | 5.40 | 7.72 |
| 15:00 | 1914 | KK Homeboyz vs Nairobi City Stars FC | 1.98 | 3.08 | 3.71 |
| 15:00 | 4528 | AFC Leopards vs Mathare United | 1.70 | 3.60 | 5.00 |
| 15:00 | 5414 | Tusker vs Vihiga Bullets FC | 1.27 | 4.75 | 9.70 |
| 15:45 | 3183 | Diagoras FC vs Ergotelis | 2.56 | 2.95 | 2.70 |
| 16:00 | 3008 | Mbeya City vs Ruvu Shooting | 1.54 | 3.59 | 5.75 |
| 16:00 | 4715 | Police FC Rwanda vs Rutsiro FC | 1.73 | 3.38 | 4.44 |
| 16:00 | 5747 | Gicumbi vs Mukura | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 16:00 | 5754 | Musanze vs Gasogi United | 2.02 | 3.13 | 3.51 |
| 17:00 | 2643 | Alanyaspor vs Hatayspor | 2.36 | 3.36 | 2.82 |
| 17:00 | 4417 | Kerala Blasters FC vs ATK Mohun Bagan | 2.74 | 3.32 | 2.30 |
| 17:50 | 3884 | Al-Ettifaq vs Abha | 1.94 | 3.56 | 3.66 |
| 17:55 | 4308 | AL Khalidiyah vs Muharraq SC | 2.70 | 3.03 | 2.50 |
| 18:00 | 2133 | Kwara United vs Kano Pillars | 1.41 | 3.71 | 8.30 |
| 18:00 | 2501 | MS Kiryat Gat W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 1.52 | 4.35 | 4.74 |
| 18:00 | 2888 | PO Xylotymbou vs Omonia Nicosia | 14.43 | 6.35 | 1.15 |
| 18:00 | 3465 | Atletic Club Escaldes vs UE Engordany | 1.33 | 4.82 | 7.13 |
| 18:00 | 5700 | Atletico San Luis U20 vs FC Juarez U20 | 1.53 | 3.94 | 5.19 |
| 18:10 | 3705 | Al Shabab Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.53 | 4.26 | 5.55 |
| 19:00 | 2200 | Ivory Coast vs Algeria | 3.23 | 3.08 | 2.30 |
| 19:00 | 4103 | Sierra Leone vs Equatorial Guinea | 3.27 | 2.87 | 2.41 |
| 20:00 | 2701 | Galatasaray vs Kasimpasa | 1.72 | 3.74 | 4.42 |
| 20:00 | 3929 | Hapoel Beer Sheva W vs Hapoel Raanana W | 1.84 | 3.96 | 3.28 |
| 20:30 | 1056 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.37 | 4.82 | 6.17 |
| 20:30 | 4434 | Al Ahli Manama vs Najma Manama | 2.40 | 3.27 | 2.64 |
| 20:45 | 4624 | PSV Eindhoven vs Telstar | 1.03 | 10.59 | 28.88 |
| 21:00 | 1681 | Elche vs Real Madrid | 5.58 | 4.28 | 1.51 |
| 21:00 | 3366 | Getafe vs Granada | 2.07 | 3.06 | 4.01 |
| 21:00 | 4933 | Santa Cruz RN vs Assu RN | 1.67 | 3.52 | 4.63 |
| 21:30 | 1683 | Bnot Netanya W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 8.63 | 6.14 | 1.22 |
| 21:30 | 5547 | Levante W vs Atletico Madrid W | 3.42 | 3.61 | 1.89 |
| 22:00 | 1909 | Gambia vs Tunisia | 4.36 | 2.97 | 1.98 |
| 22:00 | 4118 | Mali vs Mauritania | 1.37 | 4.35 | 8.90 |
| 22:30 | 1971 | Vitoria Setubal vs UD Santarem | 1.40 | 4.26 | 6.58 |
| 22:30 | 3605 | Aris Salonica vs Lamia | 1.37 | 4.24 | 7.51 |
| 22:45 | 2914 | Arsenal vs Liverpool | 3.35 | 3.45 | 2.06 |
| 22:45 | 3181 | UE Santa Coloma vs FC Ordino | 1.43 | 4.33 | 5.97 |
| 22:45 | 3485 | Hibernian vs Cove Rangers | 1.10 | 7.30 | 17.29 |
| 23:00 | 1712 | Tarxien Rainbows vs Senglea Athletic | 1.40 | 4.80 | 7.20 |
| 23:00 | 2890 | Roma vs Lecce | 1.34 | 4.93 | 7.89 |
| 23:00 | 4614 | Ajax vs Excelsior Maassluis | 1.01 | 17.33 | 77.03 |
| 23:30 | 3145 | Athletic Bilbao vs Barcelona | 3.16 | 3.21 | 2.24 |

### IJUMAA - 21/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:00 | 1057 | CD Tapatio vs Venados FC | 2.37 | 3.13 | 2.79 |
| 02:00 | 3620 | Rionegro Aguilas vs Atletico Bucaramanga | 2.17 | 3.08 | 3.18 |
| 02:00 | 3832 | Desportiva Alianca AL vs CSA AL | 4.62 | 3.27 | 1.73 |
| 04:00 | 3100 | Peru vs Jamaica | 1.42 | 4.41 | 7.62 |
| 04:05 | 1541 | America De Cali vs Envigado FC | 1.55 | 3.72 | 5.41 |
| 06:00 | 5251 | San Luis vs Juarez FC | 2.04 | 3.21 | 3.65 |
| 10:35 | 1352 | Adelaide United W vs Wellington Phoenix W | 1.12 | 7.53 | 13.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM YAFICHUA MBINU ILIYOWASAIDIA SOKOINE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza FC juzi, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Idd Aboubakar, amesema pamoja na mambo mengine, ushindi wao ulitokana na kuusoma vyema Uwanja wa Sokoine na kupanga mbinu tofauti za kuwakabili wapinzani wao.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Iddi alisema walishuka dimbani kwa tahadhari kubwa kwa sababu walielewa wanakwenda kucheza mechi kwenye uwanja ambao si rafiki, hivyo walichofanya ni kutengeneza mkakati wa kutumia mfumo ambao unaweza 'kuwabeba'.

"Tuliingia kwa tahadhari, tuliiheshimu sana Mbeya Kwanza, lakini kikubwa zaidi ni uwanja, wakati tunaawaangalia Mbeya Kwanza wanachezaje, lakini tuliangalia viwanja kwa sababu hakikuwa rafiki sana, na si kwetu tu, hata kwa wapinzani wetu, kwa hiyo tulijua ni jinsi gani ya mfumo unaoihitajika. Tukapanga ni muda gani tuwe na mpira na muda gani wa kuwaachia wapinzani wetu na sisi kukaba. Tunashukuru tumeshinda na sasa tunaangalia mechi ijayo," Iddi alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Maka Mwalwisi, alisema wamepoteza mechi hiyo nyumbani kutokana na makosa ya kawaida tu ya mchezo.

"Ni matokeo ya mpira, tumefanya kosa moja wenzetu wametuadhibu, ni kosa la kawaida la kimpira, pia tumecheza na timu kubwa," alisema Mwalwisi.

Azam imechupa hadi nafasi ya tano ikiwa imefikisha pointi 18, ikicheza mechi 12, kushinda mechi tano, sare tatu na kupoteza michezo minne wakati Mbeya Kwanza ikiwa kwenye nafasi ya 11 na pointi zake mkononi 11.



Wachezaji wa Simba Queens katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mechi zao mbili za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania walizocheza na kupata pointi sita dhidi ya Alliance Girls na TSC Queens. **PICHA: SIMBA SC**

# *Kiungo Geita Gold FC atimkia Sauzi*

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mtukutu wa Geita Gold FC, Kelvin Nashon, ameelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kufanya majaribio ya kucheza soka la kulipwa katika klabu ya Venda Football Academy.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Geita Gold, Nashon amekwenda Afrika Kusini akiwa na baraka za klabu yake na imemtakia mafanikio katika safari yake mpya.

"Uongozi wa klabu ya Geita Gold, tunapenda kumtakia kila la kheri mchezaji wetu, Kelvin Nashon Naftari katika safari yake ya majaribio, Afrika Kusini," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Nyota huyo aliondoka nchini Januari 16, mwaka huu, baada ya Geita Gold kumaliza mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Ikumbukwe kuwa hii ni timu na pia ni chuo cha soka kinacholea na kukuza vipaji kinachofanya vizuri sana nchini Afrika Kusini na barani Afrika kwa ujumla. Uongozi kwa moyo mkunjufu kabisa unamtakia kila la kheri na mafanikio, klabu ikibariki safari hiyo, kwa sababu mafanikio yake ni mafanikio ya Geita Gold na nchini kwa ujumla." Iliongeza taarifa ya klabu hiyo ya mkoani Geita.

# Michezo

Alhamisi Januari 20, 2022

Nipashe




'Wachezaji Chelsea wamechoka'

UKURASA 21

HAPA UMEFIKA...



Winga wa Yanga, Denis Kaseke (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Mbuni FC katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yaifuata Mtibwa Manungu kwa tahadhari

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha mabingwa watetezi, Simba kimeingia kambini jana, kiungo Mzambia Clatous Chama anatajwa ataiongoza timu hiyo katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Tayari Bodi ya Ligi jana ilitangaza rasmi kuufungulia Uwanja wa Manungu baada ya kufanyiwa marekebisho maalumu yaliyoelekezwa na bodi hiyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally, alisema wameshayasahau matokeo ya mechi dhidi ya Mbeya City na sasa akili na nguvu zao wamezielekeza katika kupambana kuhakikisha wanaifunga Mtibwa Sugar.

Ally alisema kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka Dar es Salaam kati ya leo na kesho kwenda Morogoro kuweka kambi ya muda mfupi na asubuhi siku ya mchezo ndio wataenda Turiani.

Aliongeza kwa kumtaja Chama atakuwa miongoni mwa kikosi kitakachoshuka dimbani katika mchezo huo kulingana na mipango na programu za benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Pablo Franco.

"Takribani ni miaka 20 Simba haijacheza kwenye Uwanja wa Manungu, hatuwezi jua kwanini tunaenda kucheza huko ila tumejipanga vizuri na tuko tayari kutafuta matokeo chanya ya pointi tatu katika mchezo huo," alisema kiongozi huyo.

Hata hivyo Ally alisema kutokana na Uwanja wa Manungu kutokuwa na uwezo wa kubeba idadi kubwa ya mashabiki, Simba inaiomba Bodi ya Ligi na watu wa usalama kuhakikisha ulinzi wa kutosha unapatikana siku hiyo ya mechi.

Aliongeza wanashangazwa na hali anayopita nahodha wao, John Bocco na sasa uongozi umeahidi kukutana na nyota huyo ili kuzungumza naye na kupata suluhisho la kumaliza 'yanayomsibu' kutokana na umuhimu wake.

# Yanga: Ligi Kuu 'ngoma mbichi'

**Na Dennis Fusi**

### ●●● Yakiri wapinzani wao 'hawajalala', hivyo wanahitaji kupambana ili...

TUMEJIPANGA. Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ambaye kikosi chake ndio kinaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo inaendelea hapa nchini.

**Yanga ina pointi 32 ikiwa imeshinda mechi 10 na kutoka sare michezo miwili wakati watani zao ambao ni mabingwa watetezi, Simba wako katika nafasi ya pili wakiwa na pointi 24, lakini wana mechi moja mkononi.**

Vinara hao wa ligi watashuka tena dimbani Jumapili kuwakabili wenyeji 'Maafande' wa Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika, Moshi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema amekuwa akiendelea kukiimarisha kikosi chake kwa sababu anahitaji kushinda kila mechi iliyoko mbele yao ili kufikia malengo.

Nabi alisema kwake kila mechi ni sawa na fainali na dhana hiyo itawasaidia kuongeza juhudi na kuwaheshimu wapinzani wao kutokana na timu zote wanazokutana nazo pia zimejipanga kusaka matokeo chanya.

Kocha huyo raia wa Tunisia alisema ushindani wa kuwania namba katika kikosi chake ni sababu nyingine ya timu yake kupata matokeo mazuri licha ya changamoto mbalimbali wanazokutana nazo.

"Tunajiandaa vizuri kuelekea katika kila mechi, tumejipanga kupata matokeo mazuri katika mechi zote tunazocheza, najua si kazi rahisi lakini hayo ndio malengo yetu makubwa, ushindi ndio hukupeleka kwenye malengo, huwezi kufikia malengo kama unapoteza mechi, ligi ni ngumu na hakuna mechi rahisi," alisema Nabi.

Aliongeza anashukuru kikosi chake kimeendelea kuimarika na wachezaji ambao walikuwa hawapati namba wamebadilika na kuongeza ushindani kwenye timu.

"Haikuwa kazi rahisi, mchezaji uliyekuwa unamtegemea anakosekana kwenye kikosi kwaa sababu ambayo uliitarajia au hukuitarajia, lakini waliobakia wanaingia kwenye kikosi cha kwanza wakiwa na ari ile ile, ni jambo la kushukuru, kila siku na kila mechi kwetu ni fainali, ninaamini tutafika," Nabi aliongeza.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Haji Manara, alisema ligi hii ni ngumu lakini ili watimize malengo yao ni lazima waungane kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo yao iliyobakia.

Manara alisema hakuna ubingwa mwepesi, ni wakati wa wao kupambana na kuzipa uzito mechi zao zote watakazocheza, lakini wasiache kumwomba Mwenyezi Mungu kwa kushinda taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa mwaka 2021/22.

"Niwaase wachezaji, benchi la ufundi, sisi viongozi, wanachama na mashabiki wa Yanga, ligi hii ni ngumu sana, hakuna ubingwa mwepesi, tuipe uzito mkubwa sana hii mechi ya Polisi, nafahamu wapinzani wetu hawatalala usingizi, niwaombe tuongeze ushirikiano," alisema Manara.

Alisema ligi bado ni 'mbichi' kwa sababu zimebaki mechi 18, hivyo vita ya kuwania taji la 28 inatakiwa kuendelea kwa kasi kubwa na kamwe hawatakiwi kubweteka licha ya sasa kuwa kileleni.

Aliongeza ushindani uliopo msimu huu ni mkubwa kwa sababu kila timu imejiimarisha na hakuna mechi ndogo au nyepesi ambayo watacheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA ambapo watakabiliana na Mbao FC kutoka jijini Mwanza kwenye hatua ya 32 Bora.

Katika kujiandaa kuwakabili Polisi Tanzania, Yanga jana ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mbuni FC ya Arusha.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >